# "UCHANGANUZI WA KIISIMU – MATINI WA *MSIMU WA TISA*"

NA

MIRIAM ATEMO STAUS MAKANGA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library
0479939 1

2008

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

______________________ 4/11/08

Miriam Atemo Staus Makanga — Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ 4-11-08

Dkt. Mwenda Mbatiah — Tarehe

(Msimamizi)

______________________ 04.11.08

Hezron Mogambi — Tarehe

(Msimamizi)

**TABARUKU**

Tasnifu hii nawatabarukia marehemu babangu Raphael Makanga na marehemu mamangu Dorina Ondeche waliolala usingizi usiojua kuamka kwa msingi thabiti walioniwekea maishani uliothamini elimu. Singefika kiwango hiki cha masomo kama siyo kwa moyo wao wa kujinyima mengi ili kufanikisha masomo yangu.

Umbali huu nimefika
Ni kwa sababu yenu baba na mama
Asante kwa kukazana bila kuchoka
Kunilea na kunitakia mema maishani
Leo hii ingekuwa bora kwenu
Kuvuna matunda ya mti mliopanda
Laleni salama wapendwa hadi tukutane tena.

## SHUKRANI

Natoa shukrani nyingi kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Nasema asante kwa neema yake iliyonipa hekima na busara wakati wa safari hii ndefu iliyokuwa na changamoto za kila aina.

Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu, Dkt. Mwenda Mbatiah na Hezron Mogambi ambao hawakuchoka kuipitia kazi hii na kuifanya ifikie kiwango hiki. Nasema asante kwa mashauri mema mlionipa.

Nawashukuru wahadhiri wengine wa Idara ya Isimu na Lugha waliochangia kuboresha masomo yangu kwa mawaidha yao. Hawa ni: Prof. Abdulaziz, M. Prof. Kithaka Mberia, Dkt. Kineene Mutiso, Dkt. John Habwe, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Wamitila Kyallo, Dkt. Tom Olali na Mukhwana Ayub. Mungu awajalie maarifa zaidi.

Kwa wenzangu tuliogelea pamoja katika bahari ya usomi nasema asante kwa ushirikiano wenu. Wakati mambo yalituwia magumu, tulihimizana kuendelea kung'ang'ana, hali iliyofanya maisha kuwa mepesi. Hawa ni: Betty Karimi, Noreen Mwalili, Reuben Kisiroche, Kenneth Nyaosi na Tola Kofa. Mungu awabariki katika kila jambo mfanyalo.

Shukrani zangu za dhati zimwendee mume wangu John Mark Udalang'. Ulijitolea kwa hali na mali kufanikisha kazi hii kutoka mwanzo hadi mwisho. Asante kwa kuwa rafiki wa kipekee na kuwa karibu nami muda huu wote wa masomo haya. Nasema asante kwa hisani yako na Mungu akubariki sana.

Sina budi kutoa shukrani jazila kwa wanangu wapendwa Valarie, Rael, Trevor na Tevian. Asante kwa uvumilivu wenu kwa muda huo wote nilipokuwa mwanafunzi na kwa kunitia motisha nikazane vilivyo. Mungu awajalie neema msome hadi kiwango hiki.

Aidha, namshukuru dadangu Betty Oyuga kwa kunihimiza kujitahidi zaidi. Mungu akujalie kila la heri maishani.

Sitasahau kuwashukuru Pam na Lydia wa Chuo Kikuu cha Nairobi waliopiga chapa kazi hii. Aidha shukrani ziwaendee wale wote waliochangia na kunifanya kukamilisha kazi hii ambao sijawataja . Nasema asante.

**IKISARI**

Tasnifu hii imeshughulikia uchanganuzi wa kiisimu-matini wa diwani ya *Msimu wa Tisa* kwa kujikita katika dhana za muala na mshikamano. Uchanganuzi huu umefanywa kwa kufuata mwelekeo wa kinadharia wa muala wa Halliday na Hasan (1976) pamoja na mwelekeo wa umatini na Beaugrande na Dressler (1981).

Utafiti huu umegawanywa katika sura nne. Katika sura ya kwanza, tumetanguliza kwa kuelezea juu ya utanzu wa ushairi huru. Tumefafanua pia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, na nadharia tete ambazo zimetumiwa katika utafiti huu. Sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka, na yaliyoandikwa kuhusu mada hii yanajitokeza pia katika sura hii. Aidha, msingi na kinadharia na njia za utafiti zinakamilisha maelezo katika sura hii.

Sura ya pili imetafiti muala katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* kwa kuchanganua vipengele vya urejelezi, udondoshaji, ubadilishaji, uunganishaji na muala wa kimsamiati na kuonyesha jinsi vinavyojenga muala. Mwishoni mwa sura hii, tumechora majedwali yanayoonyesha vipashio mbalimbali vya muala katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.*

Katika sura ya tatu, tumeanisha vipengele vya mshikamano kama vile: mpangilio wa sauti, maneno, sentensi, uhusiano wa mada, anwani na yaliyomo pamoja na muktadha na mandhari ili kubainisha namna vinavyojenga mshikamano katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.*

Sura ya nne ni hitimisho na mapendekezo ambapo tumehitimisha kwa kueleza viwango vya matumizi ya aina mbalimbali za muala. Matumizi ya vipengele vya mshikamano pia yametolewa. Hatimaye, tumemalizia utafiti huu kwa kutoa mapendekezo ya tafiti za kufanywa na tahakiki za baadaye.

## VIFUPISHO NA ISHARA

| | | |
|---|---|---|
| uk. | - | ukurasa |
| n.k. | - | na kadhalika |
| ub. | - | ubeti |
| Taz. | - | tazama |
| Ø | - | udondoshaji |
| X | - | kurejelea mara ngapi kipashio kimetumiwa |

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

Matini – mawasiliano yenye maana ya kisemantiki yaliyoandikwa au kuzungumzwa na yenye muundo na mtindo ambao waweza kuwa wa kishairi au kinathari.

Muala – dhana ya kisemantiki inayojenga matini kutokana na uhusiano wa kisarufi na wa kimsamiati ambapo kufasirika kwa kipashio kimoja kunategemea kipashio kingine.

Muktadha wa kiisimu – huu ni muktadha unaorejelea kipashio na kukihusisha na vipashio vinavyokizunguka, Werth (1984:34). Aina hii ya muktadha hutegemea uhusiano kati ya vipashio.

Muktadha wa kihali – muktadha ambao hutegemea maarifa ya awali yanayohusu mazingira nje ya matini ili kupata maana ya kipashio husika.

Urejelezi – aina ya muala inayozingatia utegemezi baina ya vipashio ambapo kufasiriwa kwa kipashio kimoja hutegemea kurejelewa kwa kipashio kingine katika matini.

Ekisofora – aina ya urejelezi unaohitaji msomaji kurejelea mazingira ya nje ili kufasiri kipashio kilichomo.

Endofora – aina ya urejelezi unaopatikana katika matini kwa vile kipashio cha urejelezi hurejelea kingine kilichomo ndani ya matini.

Anafora – urejelezi nyuma ambapo kipashio kinachofasiriwa hurejelea kipashio ambacho tayari kimetajwa.

Katafora – aina ya urejelezi ambao huhitaji msomaji asome mbele kwenye matini ili apate ufasiri wa kipashio husika.

Ubadilishaji – aina ya muala inayotokea wakati kipashio kimoja kinadondoshwa na badala yake kingine kuwekwa pasi na kubadili maana ya awali.

Udondoshaji – aina ya muala inayotokea wakati ambapo kipashio fulani katika usemi huachwa na badala ya kuwakilishwa kwa kingine huwakilishwa na umbo kapa.

Uunganishaji – aina ya muala ambayo fasiri ya kipashio haitegemei kurejelea kwingine bali nguvu za kimuala hutokana na maana ya kisemantiki ya kiunganishi husika.

Muala wa kimsamiati – aina ya muala inayohusisha uhusiano wa kimuundo baina ya kipashio na kingine.

Mshikamano – uhusiano baina ya vijenzi vya matini ambavyo hutegemea maarifa ya awali aliyonayo msomaji ili kuibua maana.

**FAHARASA**

UNGAMO ........................................................................................ ii

TABARUKU .................................................................................... iii

SHUKRANI.........................................................................................iv

IKISARI ...............................................................................................vi

VIFUPISHO NA ISHARA ............................................................. viii

MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU ................................................ix

FAHARASA .........................................................................................xi

**SURA YA KWANZA**

1.1 UTANGULIZI ......................................................................................1

1.2 TATIZO LA UTAFITI .........................................................................4

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI ..............................................................4

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII ...............................................4

1.5 NADHARIA TETE ..............................................................................5

1.6 UPEO NA MIPAKA ............................................................................5

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII ...........................................5

1.7.1 KAZI ZA KINADHARIA .................................................................7

1.7.2 KAZI ZA UCHANGANUZI WA MATINI ..........................................7

1.8 MSINGI WA KINADHARIA .................................................................9

1.9 NJIA ZA UTAFITI ...............................................................................18

TANBIHI .................................................................................................19

**SURA YA PILI**

**MUALA KATIKA *MSIMU WA TISA***

2.1 UTANGULIZI ........................................................................................20

2.2 UREJELEZI ..........................................................................................21

2.3 UDONDOSHAJI NA UBADILISHAJI ....................................................29

2.4 UUNGANISHAJI .......................................................................................31

2.5 MUALA WA KIMSAMIATI ...........................................................................37

2.6 MAJEDWALI YA VIPASHIO ........................................................................44

2.6.1 NAHODHA NA JAHAZI ..............................................................45

2.6.2 TOPE LA MIZOZO ....................................................................46

2.6.3 WEREVU .......................................................................................47

2.6.4 MSIMU WA TISA ............................................................................48

2.6.5 MSIMU MWINGINE WA WASALITI..............................................49

2.6.6 KITINI ...........................................................................................50

2.6.7 TUME ZA RAIS...............................................................................51

2.6.8 MAGENGE MATATU .......................................................................52

2.7 HITIMISHO ...............................................................................................53

TANBIHI ..........................................................................................................55

**SURA YA TATU**

**VIPENGELE VYA MSHIKAMANO KATIKA *MSIMU WA TISA***

3.1 UTANGULIZI ...............................................................................................56

3.2 MPANGILIO WA SAUTI ..................................................................................57

3.3 MPANGILIO WA MANENO...............................................................................60

3.4 MPANGILIO WA SENTENSI ....................................................................62

3.5 UHUSIANO WA ANWANI, MADA NA YALIYOMO ............................64

3.6 MUKTADHA NA MANDHARI ...............................................................66

3.7 HITIMISHO .............................................................................................69

**SURA YA NNE**

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

4.1 HITIMISHO .............................................................................................71

4.2 MAPENDEKEZO ......................................................................................75

MAREJELEO ...............................................................................................76

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Ushairi huru ni hatua ya maendeleo ya kimuundo katika utunzi wa ushairi ambao una usuli wake katika nyimbo. Mapigo ya nyimbo hizi yaliibua muundo wa vina na mizani ambayo huzingatiwa kama umbo la shairi. Ushairi wa jadi ulithamini sana namna ya kuwasilisha ujumbe kwa kuzingatia umbo ili ujumbe upatikane kama anavyosema Mazrui (1988:xii) "hapana shaka kwamba umbo la mashairi daima litakuwa na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maudhui".

Ushairi huru umefasiriwa na baadhi ya washairi kama ukiushi dhidi ya utunzi wa jadi wa mashairi kwa vile hupuuza swala la arudhi za jadi. Watunzi wa mkondo wa ushairi huru ambao pia huitwa wanamabadiliko waliona kufuata kanuni kongwe ilikuwa ni utumwa uliozuia ubunifu katika jamii zilizokuwa zinabadilika kiutamaduni nao pia walihitaji kuakisi mabadiliko hayo.[1] Mtazamo huu unaoana na mawazo ya Wamitila (2002:97) anayesema "fasihi ni hai na kitu chochote hai hubadilika na kukua". Chiraghdin (1977:3) pia amechangia swala la ukuaji wa ushairi kwa kusema mashairi "hayakukaa palepale katika ukale wake, yamebadilika kutokana na maendeleo ya mawazo ya mwanadamu. Basi kumetokea na kukua kwa bahari mbalimbali za ushairi katika hilo umbo." Ni juhudi hizi za kujiepusha na huu utumwa zilizoibua ushairi huru ambao ulimpa mtunzi uhuru wa kueleza mawazo yake kwa njia huru bila kubanwa na kufuata kaida fulani.

Kuzuka kwa ushairi huru katika ushairi wa Kiswahili kulianzisha upinzani mkubwa kutoka kwa wanamapokeo ambao walitaka shairi lifuate taratibu na kanuni fulani. Wanamabadiliko hawakuona umuhimu wa kuzingatia sheria hizo katika ushairi. Mitazamo hii inayokinzana ndiyo iliyoibua mjadala mkali ulioishia kuwa mgogoro mkubwa. Mgogoro wenyewe ulifungamana na swala la umbo la shairi ambalo huwa na mpangilio maalum wa vina, idadi sawa ya mistari na mizani. Baadhi ya wanamapokeo walidai kuwa urari wa vina na mizani ni uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili hivyo wakakataa kukubali kamwe ushairi huru kama vile anavyosema Farouk Topan katika dibaji ya *Kichomi* uk. 2 "ukosefu wa vitu hivi umewafanya wataalamu fulani wa Kiswahili wayakaripie mashairi haya, wao hawakubali kwamba haya yastahili kuitwa mashairi". Kulingana na Topan, hadhi ya ushairi haitegemei muundo au umbo fulani bali yategemea yale yasemwayo na maneno ya shairi[2]

Wasomi mbalimbali wametoa fasiri anuwai kuhusu ushairi huru. Arege (1998:1) anasema "ushairi huru ni ushairi ambao haufuati kanuni za kijadi katika utunzi wake". Kulingana naye katika ushairi huru, mshairi hajifungi katika kanuni za mtiririko wa vina, ulinganifu wa mizani na hata idadi sawa ya mishororo katika kila ubeti. Wangari (1988:51) anasema kuwa ushairi huru ulikwepa kanuni ya ujitoshelezi wa ubeti hivyo kufanya shairi kuonekana kama mkusanyiko wa msitari tu, iliyozongwa pamoja bila sababu maalum wala umoja wa maudhui.

Wamitila (2002:96) anaeleza kuwa badala ya kutegemea mizani na vina kuzua maana, inafaa kutegemea mbinu zingine kama vile mpangilio wa maneno, unyumbuaji wa

maneno, mpangilio wa sentensi katika kuzua hisia nzito katika utungo wa kishairi. Kwa mujibu wa maoni yake, hivi ndivyo vipengele vay kimsingi katika kutambulisha ushairi kwa vile ni vipashio zaidi ya vina na mizani. Ushairi huru huwa na usambamba wa kimawazo pamoja na matumizi ya urudiaji katika kiwango cha neno, virai au mistari.

Mitazamo ya baadhi ya wasomi hawa inadhihirisha kuwa ushairi huru husisitiza zaidi vigezo ambavyo hudhibiti maana na fahiwa na kupuuza umaarufu wa umbo kama kitambulisho kikuu cha utungo. Hii ni kwa sababu ushairi huru ni sehemu ya utamaduni wa jamii na umbo lake limekuzwa kupitia vipindi mbalimbali.

Ushairi huru umeendelezwa na waandishi kama vile: E. Kezilahabi: *Kichomi* (1974) na *Karibu Ndani* (1988) , K. Kahigi na M. Mulokozi: *Mashairi ya Kisasa* ( 1973) na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1979) , A. Mazrui: *Chembe cha Moyo* (1988) , K. Mutiso: *Mizani Yangu* (1986) , K. Mberia: *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001), S.A. Mohammed: *Jicho la Ndani* (2001).

Ushairi huru kama tanzu mojawapo wa fasihi andishi waweza kuchanganuliwa kiisimu-matini ili kudhihirisha kuwa ni matini. Uchanganuzi wowote wa matini kama kipashio cha lugha huzingatia muala na mshikamano kwani ni miongoni mwa viambajengo muhimu sana vya matini.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Aghalabu mashairi huru yamechanganuliwa kwa misingi ya muundo. Uchanganuzi wa kiisimu-matini ambao huzingatia mpangilio wa vipashio katika kuibua maana haujashughulikiwa katika ushairi huru. Hali hii imechangia haja ya utafiti huu unaohusu uchanganuzi wa mashairi katika diwani ya *Msimu wa Tisa* hasa kwa kuangaza vipengele vya muala na mshikamano na jinsi vinavyojenga umatini. Hivi ni kusema kwamba tunayachanganua mashairi kiisimu-matini ili kuweza kujibu swali la ikiwa yanajitosheleza kama matini.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu umeongozwa na madhumuni yafuatayo:

i. Kuchunguza aina za muala zinazojenga umatini katika *Msimu wa Tisa.*

ii. Kuchunguza aina za muala ambazo zimetumiwa sana na zile ambazo zimetumiwa kwa kiasi kidogo.

iii. Kuchunguza vipengele vya mshikamano vinavyochangia umatini katika *Msimu wa Tisa.*

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

*Msimu wa Tisa* ni diwani ya hivi majuzi na hakuna utafiti wa kiisimu-matini ambao umefanyiwa diwani hii. Aidha, kazi nyingi ambazo zimeshughulikia muala na mshikamano zimezingatia matini za Kiingereza. Baadhi ya wanaisimu ambao wameshughulikia dhana hizi walifanya hivyo katika udhahania wake bila kuzioanisha na

uandishi wa fasihi. Utafiti huu pia umechangia uhakiki wa fasihi ya Kiswahili katika mwelekeo wa kisimu-matini.

## 1.5 NADHARIA TETE

i. Baadhi ya vipengele vya muala vinatoa mchango mkubwa kuliko vingine katika kujenga umatini katika *Msimu wa Tisa.*

*ii.* Muala na mshikamano ni dhana ambazo zimechangia kuwasilisha maudhui ya *Msimu wa Tisa.*

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu unachunguza dhana za muala na mshikamano katika mashairi huru ya *Msimu wa Tisa.* Tunachanganua mashairi yanayoshughulikia maudhui ya siasa na kuonyesha aina mbalimbali za muala na mshikamano zilizomo. Vipengele vingine vya umatini kulingana na Beaugrande na Dressler (1981)ambavyo ni: dhamira, kiasi cha yaliyomo, ukubalifu, mahusiano na mwingiliano wa kimatini vitatajwa tu jinsi vinavyohusiana na muala na mshikamano wala havitafanyiwa uchanganuzi wa kiisimu – matini.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

### 1.7.1 KAZI ZA KINADHARIA

Halliday na Hasan (1976) katika kitabu chao *Cohesion in English* wameonyesha umuhimu wa muala katika matini. Wanasema kuwa muala ndicho kipengele cha kimsingi

cha kubainisha matini. Vipengele vya muala ambavyo wameshughulikia ni pamoja na urejelezi, ubadilishaji, uunganishaji, udondoshaji na muala wa kimsamiati. Kazi yao imekuwa na manufaa kwetu kwa sababu imeshughulikia muala, kipengele ambacho tunachunguza katika utafiti wetu, hivyo kutufaidi kinadharia. Hata hivyo wameshughulikia matini za Kiingereza lakini utafiti huu unashughulikia matini ya Kiswahili.

Van Dijk (1977) katika kitabu chake *Text and Context* ameshughulikia matini na muktadha. Licha ya kazi yake kushughulikia matini za Kiingereza, mchango wake ni muhimu katika kazi yetu kwa sababu ameshughulikia dhana ya mshikamano kwa kueleza jinsi muktadha huchangia kukuza mshikamano. Maoni yake juu ya muktadha yametuelekeza katika utafiti huu.

Leech na Short (1981) wametafiti muala katika matini za Kiingereza katika kitabu chao *Style in Fiction.* Wameonyesha jinsi muala hukuza umatini. Kazi yao imekuwa na manufaa kwetu kwa vile imetupa mwelekeo wa kinadharia wa kuchunguza muala katika matini. Tofauti na utafiti wetu unaoshughulikia matini ya kifasihi ya Kiswahili, wao walishughulikia matini za Kiingereza.

Beaugrande na Dressler (1981) katika *Introduction to Text Linguistics* wameshughulikia sifa bainifu za kuchanganulia matini yoyote ile. Wamechunguza kwa kina dhana za muala na mshikamano kama vipengele vinavyochangia uainishaji wa kazi fulani kama matini. Wahakiki hawa wamechangia utafiti huu kwa upande wa nadharia kwa

kushughulikia matini za Kiingereza. Utafiti wao unatofautiana na wetu kwa sababu haujachunguza matini ya kifasihi ambayo tunashughulikia.

Yule (1996) ameshughulikia mshikamano katika kitabu chake cha *Pragmatics*. Kazi yake imechunguza matini za Kiingereza na kufafanua vipengle vinavyojenga mshikamano katika matini. Mwelekeo wake umekuwa na manufaa kwetu kwa sababu ameangazia dhana ya mshikamano, kipengele cha matini ambacho utafiti huu unachunguza.

Neubert na Shreve (1992) katika kitabu chao cha *Translation as a Text* wameshughulikia vipengele vya matini kama vilivyoshughulikiwa na Beaugrande na Dressler (1981). Kazi yao imekuwa na manufaa kwetu kwa vile imechunguza muala na mshikamano katika kufanikisha matini ya fasihi tafsiri. Kazi hii imetupa mwelekeo wa kuichanganulia matini ya *Msimu wa Tisa* ingawa wao walichunguza matini za Kiingereza.

## 1.7.2 KAZI ZA UCHANGANUZI WA MATINI

Habwe (1999) katika tasnifu yake ya uzamifu "Discourse Analysis of Kiswahili Political Speeches" ametafiti muala katika hotuba za kisiasa. Amechunguza jinsi ambavyo muala hutumika katika hotuba na kufanya hotuba kuwa na muumano. Ingawa kazi yake imeshughulikia muala katika mazungumzo, imetupa mwongozo wa kuchanganua muala katika mashairi. Utafiti wetu unaoshughulikia matini ya kifasihi andishi huenda ukadhihirisha matumizi ya muala na mshikamano kwa njia tofauti na ile ya mazungumzo.

Onguko (1999) katika tasnifu yake ya uzamili "A comparative study of Cohesion in Academic and Newspaper Texts" amechunguza muala kwa kulinganisha vipengele vya muala katika matini za kiusomi na matini za magazeti. Kazi hii imetupa mwanga wa kuchanganua muala kwa vile inahusika na kazi mahsusi. Hata hivyo jinsi muala inavyojitokeza katika kazi yake inatofautiana na jinsi ilivyo katika shairi huru kwa sababu hizi ni kazi za tanzu tofauti za uandishi. Aidha, ameshughulikia muala kwa kulinganisha nyanja mbili tofauti za maandishi ya Kiingereza. Utafiti wetu unachunguza muala na mshikamano bila ulinganisho wowote katika matini ya kifasihi.

Wangari (1988) katika tasnifu yake ya uzamili "New Trends in Ushairi" amechunguza mabadiliko katika ushairi. Kazi yake imechangia utafiti wetu kwa sababu ushairi wa Kithaka Mberia ambaye ni mwandishi wa kazi tunayochunguza umeshughulikiwa kiasi. Hata hivyo, yeye amejikita sana kwenye ufafanuzi wa mashairi haya kimuundo na kimtindo ilhali utafiti wetu unachanganua mashairi huru ya Kithaka Mberia kwa kuzingatia muala na mshikamano.

Njue (1989) katika tasnifu yake ya uzamili " Muala katika Kiswahili: Umuhimu wake katika uchambuzi wa ngano" amechanganua aina mbalimbali za muala na kuonyesha jinsi zinavyojitokeza katika ngano. Uchanganuzi wake umetupatia mwelekeo kwa sababu ameshughulikia kazi ya kifasihi. Hata hivyo, uchunguzi wake uliegemea kwenye ngano kama aina ya fasihi simulizi ilhali utafiti wetu unashughulikia kazi ya fasihi andishi.

Nzuki (2003) katika tasnifu yake ya uzamili "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka Mberia" amechunguza aina mpya za fani ambazo zimetumiwa katika ushairi huru na jinsi ambavyo zimechangia kukuza maudhui. Kazi yake imechangia utafiti wetu kwa vile imeshughulikia mtindo mpya wa uandishi ambao ni sifa mojawapo ya ushairi huru wa mwandishi ambaye mashairi yake tunachanganua.

Mulila (2005) amechanganua muala na mshikamano katika tasnifu yake ya uzamili "Muala na Mshikamano katika Kiswahili. Umuhimu wake katika uchanganuzi wa riwaya ya *Vipuli vya Figo*". Ameonyesha jinsi riwaya kama kazi ya nathari hutumia muala na jinsi mshikamano umejengwa katika matini za kiriwaya. Uchanganuzi huu umetupatia mwelekeo mzuri wa kuchanganua kazi yetu kwa vile umeshughulikia dhana tunazochunguza katika fasihi andishi. Hata hivyo ushairi na riwaya ni tanzu mbili tofauti za fasihi andishi zilizo na matumizi tofauti ya lugha hivyo muala na mshikamano kujitokeza kwa njia tofauti.

## 1.8 MSINGI WA KINADHARIA

Mwelekeo wa kinadharia unaoongoza utafiti huu umefafanuliwa na Beaugrande na Dressler (1981), Brown na Yule (1983) na Neubert na Shreve (1992) lakini ni Halliday na Hasan (1976) ambao wameupa muala mwelekeo wa kinadharia. Mwelekeo huu wa kimuala huonyesha muumano na mshikamano katika matini na huweza kutumiwa kuchanganulia kazi za kifasihi kimtindo. Mtazamo huu wa kinadharia ni muhimu katika kuchanganulia mbinu za kimuala katika kazi hii na kuitambulisha kama matini iliyo na maana.

Kulingana na Halliday na Hasan (1976), muala ndicho kipengele cha pekee cha kutambulisha matini. Wameeleza kuwa kuna aina moja ya uhusiano wa kimaana unaojenga matini ambapo faridi inafasiriwa kwa kurejelea faridi nyingine. Kwao muala huundwa wakati kufasirika kwa kipashio kimoja kunategemea kipashio kingine, hali inayosababisha uhusiano kati ya faridi inayotajwa na ile iliyotajwa awali au itakayotajwa baadaye. Utegemezi wa aina hii ndiyo unaibua maana katika matini na kujenga muala. Aidha, muala ni dhana ya kisemantiki kwa sababu hueleza uhusiano wa kimaana unaopatikana katika matini na usiohusika na muundo. Muundo wa sentensi moja unaweza kuleta muala, hasa muundo wa sentensi za Kiswahili ambao hulazimu kuwepo kwa viambishi awali vya vitenzi ambavyo hupatanisha nomino au kiwakilishi chake na vipashio vingine.

Halliday na Hasan (1976) wameonyesha uhusiano baina ya vipashio vya sentensi na siyo tu sentensi bali pia hushughulikia matini kwa jumla kama kipashio kikubwa kuliko sentensi. Vipengele ambavyo hutofautiana kimuundo huunganishwa pamoja kwa sababu ya kutegemeana kwake na kufasiriwa kama kimoja. Vipashio visivyohusiana kimaana hata kama vina muundo sawa havina muala lakini vipashio ambavyo huenda visihusiane kimuundo huungwa pamoja kupitia kutegemeana kwa ufasiri wao ili kuleta maana fulani. Hivyo sentensi zenye miundo tofauti huunganishwa kuwa kipashio kimoja chenye maana kwa sababu ya kufasiriwa kwa pamoja na muala.

Mtazamo wa Halliday na Hasan (1976) una aina tano za muala ambazo ndizo msingi wa maana katika matini nazo ni : urejelezi, ubadilishaji, udondoshaji, uunganishaji na muala wa kimsamiati.

Urejelezi huzingatia utegemezi ambapo kufasiriwa kwa faridi hutegemea kurejelewa kwa faridi nyingine katika matini. Kulingana na Halliday na Hasan (1976: 31) katika urejelezi ujumbe huendelezwa kwa jambo lile kutokea katika usemi mara ya pili au zaidi kupitia vitambulishi vya kisarufi kama kile viambishi na viwakilishi. Urejelezi si wa vipashio tu katika sentensi bali sentensi inaweza kuwa na muumano na sentensi nyingine katika matini ikiwa ina faridi zinazorejelea sentensi hiyo nyingine. Kulingana na Mulila (2005:50) kirejelezi na kirejelewa lazima viwe na sifa sawa za kisemantiki lakini si lazima viwe na muundo sawa wa kisarufi. Hii ni kwa sababu uhusiano baina yao ni wa kisemantiki, mathalan ikiwa kirejelewa ni nomino, kirejelezi chaweza kuwa kiwakilishi cha nomino mradi vyote vina sifa sawa za kisemantiki.

Kuna aina mbili za urejelezi ambazo hutegemea muktadha ili kupata maana. Kwanza ni ekisofora, urejelezi ambao Halliday na Hasan (1976:18) wanaeleza kuwa hauna nguvu za kimuala kwa vile haunganishi faridi hizi mbili (kirejelewa na kirejelezi) kama kiungo kimoja cha matini. Maana katika urejelezi wa aina hii hutegemea muktadha nje ya matini. Aidha, aina hii ya urejelezi hufaa sana katika mazungumzo ambapo mzungumzaji na msikilizaji huelewa kinachorejelewa bila utata wowote katika mazingira ya mazungumzo kwa vile wana maarifa sawa kuhusu mazingira yao.


Urejelezi wa pili ni endofora ambao ni wa aina mbili: anafora na katafora na hutegemea mazingira ya ndani ya matini katika kupata maana. Mathalan:

Watu <u>wa</u>natererekea<br>
Damu <u>i</u>natiririka<br>
Uhai <u>u</u>naporomoka

(Bara Jingine uk. 6)

Katika ubeti huu uelewa wa viambishi vilivyopigwa mistari unapatikana kwa kurejea kwa nomino inayotangulia. Kufasirika kwa kiambishi **wa** kunapatikana kwa kurejea nyuma kwa **watu,** kiambishi **i** kinafasirika kwa kurejelea **damu**, nacho kiambishi **u** kinaeleweka kurejelea nomino **uhai.**

Halliday na Hasan (1976:33) wameonyesha aina za urejelezi kimchoro kama ifuatavyo:




Urejelezi hudhihirika pia kupitia kwa viambishi ambavyo hutegemea muundo wa vitenzi na ngeli ya nomino husika. Tazama mfano huu:

Akili yangu
Huona vidonda virefu ambavyo
Vimejaa usaha
Moto wa uchungu

(Bara Jingine uk. 61)

Katika mfano huu, **vi** ni kiambishi cha nomino cha ngeli ya nane katika wingi. Upatanisho huu wa kimofosintaksia unaojenga muala umetokana na nomino ya ngeli na kiambishi chake.

Viwakilishi nafsi huru pia huonyesha urejelezi. Viwakilishi nafsi huru huwa kwa umoja na wingi, navyo ni: **mimi** na **sisi**, **wewe** na **nyinyi**, **yeye** na **wao.** Viwakilishi nafsi viambata pia huchangia urejelezi na hupatikana kwa umoja na wingi kama ufuatavyo: **ni** na **tu, u** na **m** na hatimaye **a** na **wa**. Mfano ufuatao unaonyesha urejelezi wa viwakilishi nafsi viambata.

Lulu ukingoni mwa njia
Wewe <u>u</u>ogopaye maji ya chumvi
Wewe <u>u</u>kwepaye maji ya matope
Lulu makasha – makasha
Umekuaje mmiliki

(Mchezo wa karata uk. 16)

Katika ubeti huu fasiri ya kiwakilishi nafsi kiambata **u** inapatikana kwa kurejelea kwa viwakilishi nafsi **wewe**. Viwakilishi hivi viwili vinarejelea wazo moja.

Kiwango kingine cha muala ni ubadilishaji ambao hutokea wakati kipashio kimoja kinatumika badala ya kingine ili kuepuka kurudiarudia maneno. Ubadilishaji huweza kuathiri neno au kishazi. Aidha, ubadilishaji hurejelea uhusiano wa kimsamiati kwa kushughulikia vipashio vya muundo kama vile maneno na virai, tofauti na urejelezi ambao hurejelea uhusiano wa kimaana. Katika ubadilishaji, faridi badilishi huwa na kazi moja ya kimuundo na faridi inayobadilishana nayo, hivyo kipashio kilichobadilishwa na

kile cha awali hufasiriwa kwa kurejelea kile cha awali na kujenga umatini. Ubadilishaji waweza kuwa wa nomino, kitenzi au kishazi nacho kibadala chaweza kuwa na uamilifu wa nomino, kitenzi hata kishazi.

Katika udondoshaji, kuna kipashio kinachoachwa bila kuandikwa kwa vile huwa kimendondolewa kwenye matini. Udondoshaji wa kipashio katika sentensi hausababishi utata wowote kwa vile sentensi bado hueleweka kwa kurejelea kipashio cha awali. Udondoshaji hujitokeza kama aina ya ubadilishaji usiodhihirisha kipashio cha ubadilishaji. Kama ubadilishaji, udondoshaji ni uhusiano uliomo kwenye matini unaokuza muala na kufanikisha ufasiri kwa vile kipashio kilichoachwa kimuundo hutulazimu kurejelea kwingine kupata ufasiri wake. Udondoshaji waweza kuwa wa nomino, kitenzi au hata kishazi .

Muala katika matini huweza kutokea kwa uunganishaji. Viunganishi hutoa maana fulani na kujenga muala kwa kuunganisha vipashio katika matini. Maana ya kiunganishi husababisha muala kwa kudokeza kuwepo kwa vipashio vingine vya awali. Kwa kuunganisha vipashio viwili au zaidi, uunganishaji huchangia kukuza muala na kuendeleza matukio. Uainishaji wa viunganishi hutegemea aina ya maana inayotolewa na kiunganishi.

Kulingana na Halliday na Hasan (1976:308) kuna aina zifuatazo za uunganishaji. Uunganishaji wa kinyume ambao hutoa maana kuwa wazo halijatokea jinsi lilivyotarajiwa. Uunganishaji wa aina hii huwa na nguvu za kimuala kwa kuendeleza

hoja mbili zinazokinzana. Viunganishi vya aina hii ni maneno kama: lakini, ingawa, hata hivyo, japo, ijapokuwa n.k.

Muala pia huundwa kutokana na uunganishaji wa kusababishwa kwa matukio. Uunganishaji wa aina hii huwa na maneno yenye nguvu za kimuala kama: kwa sababu, kwa hivyo basi, kwa vile n.k ambayo huunganisha wazo katika sentensi ya pili na lile katika sentensi ya kwanza. Aina nyingine ya uunganishaji ni ile ya kuongezea jambo inayoonyesha mfuatano wa matukio. Viunganishi vinavyoelezea hali ya kuongezea ni kama: na, vilevile, pia, mbali na, fauka ya n.k. Uunganishaji wa aina hii huunda muala kwa vile wazo au jambo katika sentensi ya kwanza linaendelezwa kwa kuongezewa lingine katika sentensi ya pili. Uunganishaji unaotegemea wakati hudhihirika wakati muala unaendelezwa kwa kutokea kwa tukio la pili baada ya mpito wa wakati. Viunganishi vinavyodhihirisha wakati ni kama: baadaye, kisha, halafu, baada ya n.k.

Muala wa kimsamiati hudhihirika kupitia uteuzi wa msamiati na huonyesha uhusiano wa maneno. Aina hii ya muala hujitokeza wakati msamiati ambao unahusiana unatumiwa katika sentensi zinazofuatana. Uhusiano huu husababisha muala kwa vile hakuna kurejelea kwingine kwenye matini ili kupata fasiri. Uteuzi wa msamiati unaofungamana na mada yake ni muhimu katika kuibua muala wa msamiati. Uteuzi huu wa msamiati huleta uthabiti wa matini pamoja na kuitofautisha matini na nyingine.

Muala wa kimsamiati waweza kujitokeza kupitia urudiaji. Katika urudiaji kipashio kinarudiwa kizima au kisehemu. Aidha, neno moja laweza kurudiwa kurejelea lile la

awali hivyo kuunda muala. Urudiaji wa aina hii hujitokeza sana katika matini zenye usimulizi wa nafsi ya tatu ambapo kuna wahusika zaidi ya mmoja.
Mbinu ya usambamba pia hukuza muala wa kimsamiati kwa sababu dhana moja huelezwa kwa kutumia maneno tofauti hali inayofanya matini kufasiriwa kama kitu kimoja. Muala wa kimsamiati pia hujengwa kwa kutumia sinomia, antonimia na hata hiponimia.

Matumizi ya maneno yanayokaribiana kimaana au yanayolandana pia hukuza muala wa kimsamiati. Matumizi ya msamiati ambao kila wakati hulandana pamoja hujenga muumano katika matini kwa vile unahusiana. Mathalan:

> Katika mashindano hayo, wavulana waliibuka washindi kwa kuwafunga wasichana mabao sita kwa nunge.

Katika sentensi hii, maneno yaliyopigiwa mstari huandamana na hukuza muala kwa vile yanahusishwa na wazo moja. **Wavulana** na **wasichana** ni msamiati unaohusiana na hurejelea jinsia.

Muktadha ni kipengele muhimu kinachochangia kukuza muala. Maana halisi ya neno hupatikana kwa kuzingatia muktadha. Kuna aina mbili za muktadha. Muktadha wa kihali ambao huenda nje ya matini ili fasiri ya kipashio ipatikane na muktadha wa kiisimu unaohusiana sana na muala na hushughulikia uhusiano kati ya vipashio. Kila matini huwa na muktadha wake wa kiisimu tofauti na matini nyingine.

Dhana ya mshikamano imeshughulikiwa kwa kuzingatia mtazamo wa Beaugrande na Dressler (1981). Mtazamo huu wa umatini huonyesha kuwa pamoja na muala kuna kaida zingine za matini kama vile mshikamano ambazo ni muhimu katika uchanganuzi wa matini. Kama anavyosema Crystal (1997:119) kuwa matini inastahili kuwa na muala na mshikamano ndiposa mada na uhusiano baina ya vipashio uingiliane ili kuibua maana.

Mtazamo wa umatini hushughulikia uhusiano wa vipashio vya kisarufi katika kuonyesha muumano wa matini. Pamoja na uhusiano wa vipashio vya sarufi, umatini huzingatia mpangilio wa sauti, maneno na sentensi, uhusiano kati ya anwani, mada na yaliyomo pia muktadha wa kihali na mandhari yanavyochangia kujenga mshikamano. Uhusiano baina ya wahusika na matukio pia huonyesha kiwango cha mshikamano katika matini.

Kulingana na Blakemore (1987:105) upungufu wa wazo hutegemea msomaji kujijazia kwa kurejelea maarifa ya awali au muktadha. Ni kwa mtazamo huu ambapo misingi ya mshikamano imewekwa kwenye uzoefu na maarifa ya awali hivi kwamba fasiri hutolewa kwa kuhusisha mambo tuliyozoea. Tunapotumia mtazamo huu, inadhihirika kuwa matini haijengwi tu na muktadha wa kiisimu bali pia na muktadha wa kihali ambao kwa kiasi kikubwa huchangia ufasiri wa maana katika matini.

Yule (1985:141) anaeleza kuwa fasiri ya matini haitegemei uhusiano baina ya maneno tu; kwa vile kuna jambo linalotuelekeza kutofautisha kati ya matini iliyo na muumano na ile ambayo haina muumano. Jambo hili ni mshikamano. Ingawa uhusiano wa kisarufi huchangia kuleta maana ya matini, uhusiano huu pekee hautoshi kuipa matini ufasiri.

Uhusiano wa kisarufi hurejelea maneno, virai, vishazi na sentensi kwa jumla. Uhusiano huu wa vipashio hukuza mshikamano kwa vile ufasiri wa kipashio kimoja hutegemea kingine. Utegemezi wa aina hii hujenga muumano wa matini husika. Aidha, uhusiano wa kisarufi humwezesha msomaji kufuatilia matukio na kuelewa jinsi yanavyohusiana.

Mtazamo wa Beaugrande na Dressler (1981) umechangia pakubwa katika kuonyesha uhusiano kati ya muala na mshikamano katika kujenga umatini. Kwa vile utafiti huu unahusu uchanganuzi wa dhana hizi, nia yetu ni kubainisha jinsi vipengele hivi vinategemeana kuleta maana katika mashairi huru ya *Msimu wa Tisa*.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu umefanyika kwenye maktaba. Tumesoma vitabu mbalimbali vinavyoshughulikia dhana za muala na mshikamano. Aidha, tumesoma vitabu vinavyohusiana na kaida za matini. Tumesoma pia diwani ya *Msimu wa Tisa* ili tuweze kubainisha vipengele vya muala na mshikamano vilivyomo. Katika kusoma diwani hii, tunatarajia kuonyesha takwimu za aina mbalimbali za muala na kudhihirisha jinsi mshikamano unavyojitokeza katika mashairi haya pamoja na kukuza umatini. Tumesoma pia diwani zingine za mashairi huru ili kulinganisha *Msimu wa Tisa* na matini nyingine za aina yake.

## TANBIHI

1. Taz Mazrui A. 1988, *Chembe cha Moyo*, Nairobi, Heinemann Kenya Limited, uk viii.
2. Taz Kezilahabi E. 1974, *Kichomi,* Nairobi, Heinemann Educational Books Limited, uk x.

# SURA YA PILI

# MUALA KATIKA *MSIMU WA TISA*

## 2.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyotangulia, tumefafanua vipengele vya muala na mshikamano na kuonyesha jinsi vinavyojidhihirisha katika matini yoyote ile. Katika sura hii, tunashughulikia kipengele cha muala na kuonyesha namna kinavyojenga umatini katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.* Uchanganuzi huu umetumia vipengele vya muala kama vilivyopendekezwa na Halliday na Hasan (1976).

Mwelekeo huu wa muala husisitiza kufasirika kwa vipashio mbalimbali vya matini kwa kutegemeana, hali ambayo huibua maana na kufanya matini kuwa kitu kimoja. Aina hii ya muala hujidhihirisha kwa vipashio vya kisarufi pamoja na msamiati ambao huibua maana katika matini.

Katika kuchanganua mashairi ya diwani ya *Msimu wa Tisa,* nia ni kueleza maana za kisemantiki zinazowasilishwa na aina mbalimbali za muala. Aidha, tumechunguza namna beti mbalimbali za matini hii zinapata fasiri tofauti kutokana na uhusiano baina ya maneno yanayozijenga. Uchanganuzi wa matini hii kimuala unaazimia kuonyesha uamilifu wa uhusiano wa kisarufi na msamiati katika kuibua maana mbalimbali za matini.

Katika kuchanganua matini hii, tumeonyesha vipashio vinavyosababisha muala katika mashairi husika na kubainisha aina ya muala inayojitokeza. Aidha, tumechunguza dhima ya kila mojawapo ya aina za muala katika kusawiri maudhui na matukio ya matini hii. Hatimaye tumetumia jedwali kuonyesha kipashio kinachosababisha muala katika kila ubeti, aina ya muala inayojitokeza na kipashio kinachorejelewa. Mpangilio huu umetuwezesha kujua aina ipi ya muala ambayo imetumiwa sana na ipi imetumiwa kwa kiasi kidogo katika mashairi haya. Aidha, tumeweza kujua utegemezi uliopo baina ya aina hizi za muala.

## 2.2 UREJELEZI

Urejelezi ambao ni aina ya muala inayohusisha utegemezi baina ya vipashio umetumiwa kwa wingi katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.* Aidha, urejelezi wa kiendofora ndiyo umetumiwa sana katika mashairi ya matini hii kwa vile fasiri ya kila kipashio imepatikana katika matini. Katika kuzingatia maana kupatikana ndani ya matini, urejelezi wa kianafora umetumiwa sana. Urejelezi wa aina hii umefanikisha kuunga pamoja na kuendeleza matukio hivyo kuwezesha uelewa wa mfuatano wa matukio yenyewe na kupata maana ipasavyo.

Viambishi ndivyo vimechangia pakubwa kujenga muala katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.* Mathalan:

Nahodha angemakinika kwenye usukani
Wasaidizi wake wangelidhibiti matanga
Jahazi halingelidumu kwenye mlango wa bahari
Likisukwasukwa na mawimbi yanayozozana
(ub. 2 wa "Nahodha na Jahazi")

Katika ubeti huu, fasiri ya kiambishi **a** inapatikana kwa kurejea nyuma kwa **nahodha,** kiambishi **wa** katika mshororo wa pili kinaeleweka tunaporudi nyuma kwa **wasaidizi** nacho kiambishi **li** kinapata fasiri kutokana na nomino **jahazi.** Kiambishi **ya** kinafasirika kwa kurejelea nyuma kwa nomino **mawimbi**. Virejelezi hivi vina sifa sawa kisemantiki na nomino zinazorejelewa. Mfano mwingine:

Serikali iliyoingia ikibeba vibuyu vya ahadi za asali
Ikivaa gwanda pendezi lenye rangi za upinde wa mvua
( ub wa 1 wa "Tope la Mizozo")

Matumizi ya viambishi ambavyo vimepigiwa mstari vimejenga muala pamoja na kukuza takriri katika ubeti huu. Fasiri ya kiambishi **i** inapatikana tu kwa kurejelea nyuma kwa nomino **serikali**. Fasiri hii inapopatikana inajenga muala ambao umechangia kukuza wazo moja linalohusu sifa za serikali mpya. Mfano mwingine wa urejelezi ni:

Wahuni wakigeni wamekaribishwa nchini kwa siri
Na kupewa vyeo vikuu na funguo za milango ya chuma,
Wameishi starehe wakijinaki kwa maneno yenye uvumba
Wakitishia polisi kwa mbwa wakali katika kasri zao.
( ub 7 wa "Tope la Mizozo")

Katika mishororo hii, kiambishi **wa** kinaeleweka kwa kurejelea nyuma. Fasiri mbili zinapatikana kwa kutumia kiambishi **wa** kwa kurejelea nomino inayotangulia. **Wa** ya kwanza, pili, tatu na nne inarejelea **mamluki** na imetumiwa kuelezea sifa zao lakini **wa** ya tano inayorejelea **mbwa** inakuza wazo tofauti linalohusika na sifa za mbwa wa hao

**mamluki**. Pamoja na kujenga muala, matumizi ya kiambishi **wa** ambacho kimerudiwarudiwa yamechangia katika kukuza mtiririko wa ubeti huu. Tutazame mfano ufuatao:

Vitambakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
Utaziona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao.
Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili
Watalewesha watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
("Msimu Mwingine wa Wasaliti")

Ubeti huu umetumia urejelezi wa kianafora kwa wingi. Kiambishi nafsi **wa** kinafasirika kwa kurejelea nomino **vitambakwira**. Kimilikishi **zao** kinafasirika kwa kurejelea nomino hiyo hivyo kufuma ubeti huu pamoja. Matumizi ya urejelezi wa aina hii yamechangia katika kueleza sifa za wahusika hawa (vitambakwira) ambao wamesawiriwa kama wajanja. Aidha, urudiaji wa kiambishi **wa** umechangia kukuza mtiririko katika shairi hili. Mfano mwingine:

Alipotanabahi kuwa chombo chake kilikuwa taabani
Ukweli wa siasa mbaya ya kutumia na kutupa jaani.
Ulipommulika machoni kwa mwangaza wa ufahamu
Alijibambua ngozi kuukuu kama nyoka mjanja
Akaingia uwanjani kwa mwili uliometameta
Akipiga pembe adimu ya mkombozi wa umme
( ub 2. wa "Kitini")

Viambishi vilivyopigiwa mstari vinadhihirisha matumizi ya urejelezi wa kianafora. Kiambishi nafsi **a** ambacho kimerudiwarudiwa na kimechangia kujenga takriri ya ubeti

wa pili kinafasirika kwa kurejelea nomino **waziri** ambayo imetajwa katika ubeti wa kwanza wa shairi hili. Huu ni uthibitisho kuwa hizi ni beti za matini moja. Wazo ambalo linaibuka kutokana na urejelezi wa kiambishi hiki ni tabia za waziri ambazo zinakuza maudhui ya ubinafsi na ujanja. Hii ni kwa sababu waziri anapogundua siasa zake si nzuri, anabadilisha mara moja vitendo vyake ili afaidike. Kiambishi hiki kinaendeleza wazo hili moja katika ubeti huu, hali inayodhihirisha uthabiti wa shairi hili. Kiambishi **ki** kinapata fasiri kwa kurejelea nomino **chombo** nacho kiambishi **u** kinafasirika kwa kurejelea nomino **mwili.** Viambishi hivi vyote vinakuza dhana moja na kujenga muala.

Kiambishi nafsi **tu** kimetumiwa katika baadhi ya mashairi kurejelea mwandishi pamoja na wahusika waliomo katika mashairi haya kama pasona katika ushairi. Fasiri ya kiambishi **tu** inapatikana kwa kurejelea muktadha wa kihali. Shairi la "Tume za Rais" lina matumizi haya katika mfano ufuatao:

Tumnunulie kila mwanatume Hummer
(ub. 1 Mshororo 2)
Tumjengee kila mwanatume kasri
(ub. 2 mshororo 2)
Tuitengee nusu ya akiba ya Banki kuu
(ub 3 mshororo 2)
Tuilipe kwa mkopo kutoka vitanzi vya Breton Woods

Katika shairi hili, kiambishi nafsi **tu** kimetumiwa kueleza wazo kuwa gharama inayopatikana kwa kutunza tume za rais ni wajibu wa mwandishi pamoja na wahusika waliomo kwenye shairi.

Mfano mwingine:

Tukanengukanenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele

( ub.1 mshororo 3)

Tukajijeruhi kwa kuimba "Juu! Juu! Juu sana!"

(ub.2 mshororo 3)

Tukaamini wimbo, "Yote yawezekana bila mfalme wa nzige"

(ub 3 mshororo 3)

Kiambishi nafsi **tu** katika shairi la "Magenge Matatu" kinapata fasiri kwa kurejelea mwandishi na wahusika ambao kila wakati walishirikiana pamoja katika kukaribisha uongozi mpya bila kujua hatima ya uongozi huo. Mfano mwingine:

Tulipoguna kwa maumivu makali kwenye misuli
Juhudi za kizalendo zilipopamba moto yakini
Tulipotokwa na michirizi ya jasho tukisaka utu
Tulipopambana na dhiki ya giza la miongo miwili.

(ub 1 wa "Kitini")

Katika ubeti huu kiambishi nafsi **tu** kinadhihirisha umoja wa wahusika katika kupigania ukombozi wao.

Katika shairi la **Tume za Rais,** matumizi ya kiambishi **i** katika ubeti wa kwanza, pili na tatu yamedhihirisha urejelezi wa kianafora. Kiambishi hiki kimerudiwarudiwa katika beti zote na kinafasirika kwa kurejelea nyuma kwenye nomino **tume ya rais** hivyo kukuza uthabiti wa shairi kama ifuatavyo:

Ichunguze kama njaa inaweza kuua (ub. 1 mshororo 3)
Ihariri taarifa ya tume ya rais (ub 1 mshororo 3)

Ichunguze jina la Rais wa Jamhuri (ub 2 mshororo 3)
Imtangazie Rais jina la Rais (ub 2 mshororo 5)

Tuitengee nusu ya akiba ya Banki kuu (ub 3 mshororo 3)
Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais (ub 3 mshororo 3)
Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais (ub 3 mshororo 5)

Vivumishi pia vimetumiwa katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* kudhihirisha urejelezi. Matumizi ya vivumishi vimilikishi yamechangia kujenga muala pamoja na kufafanua dhana zinazozungumziwa hivyo kuibua maana. Tazama mifano hii:

Nahodha angelimakinika kwenye usukani
Wasaidizi wake wangelidhibiti matanga
(ub 2 wa "Nahodha na Jahazi")

Katika mishororo hii, kimilikishi **wake** kinaeleweka kwa kurejelea nyuma kwenye nomino **nahodha,** hali ambayo imejenga muala kwa vile wazo la kuonyesha anayehusika limejitokeza kupitia kwa kimilikishi hiki. Mfano mwingine uliotumia vivumishi ni:

Wakitumia genge la wahuni wenye dharau kwa wenyeji
Mamluki wenye lugha inayonuka kama samaki waliooza.
Wale tuliopatia wadhifa wa kutulinda pamoja na mali zetu
Wamevamia haki zetu kwa kichaa cha usiku wa maneno
(ub 6 "Tope la Mizozo")

Ubeti huu una urejelezi wa kianafora ambao umetumia vivumishi mbalimbali. Matumizi ya kivumishi **wenye** kinafasirika kwa kurejelea nomino **wahuni** na kimetumiwa ili kutoa ufafanuzi zaidi. Viashiria pia hudhihirisha urejelezi kwa kuonyesha kinachorejelewa. Katika ubeti huu, kiashiria **wale** kimejenga muala kwa vile hatuna budi kurejea nyuma kujua wanaorejelewa ni kina nani . Kiashiria hiki na kirejelewa chake vina wazo moja la kuonyesha uhusika na vimefuma ubeti huu pamoja. Matumizi mengine ya kimilikishi kinachojenga muala ni katika mfano huu:

> Muulizaji hayumo miongoni mwa wachache ukumbini.
> Ameketi hoteli akipumbaza vizuu wake kwa vinywaji
> (ub 10 wa "Msimu wa Tisa")

Kivumishi **wake** kinaeleweka kwa kurejea nyuma kwenye nomino **muulizaji** inayoonyesha mwenye umiliki. Kurejea nyuma kunakuza muala na kuonyesha kuwa ni wazo moja linaloelezwa kwa sababu **wake** na **muulizaji** hurejelea wazo la uhusika.

Urejelezi wa kikatafora umetumika katika baadhi ya mashairi. Urejelezi wa aina hii humpa masomaji hamu ya kuendelea kusoma ili kupata fasiri ya kipashio husika. Ubeti wa kwanza wa shairi la "Werevu" umedhihirisha urejelezi wa aina hii. Katika ubeti huu, kiambishi nafsi **a** kinapata fasiri yake katika ubeti wa pili tunapogundua kuwa kinamrejelea **mgavi.** Fasiri hii imechangia kujenga muala katika shairi hili kwa sababu kiambishi nafsi **a** kinarejelea **mgavi** hivyo ni wazo moja na inaonyesha muumano katika shairi hili. Tazama mfano huu:

Angalipuuza mashauri ya wajanja waliomzunguka
Na kuthamini maana ya maneno ya wimbo wa taifa.
Angalizingatia kanuni za mkataba wa majemedari
Silaha iliyokomboa taifa kutoka minyororo ya huzuni.
Angalifahamu uaminifu ni akiba inayozaa matunda
Na kukubali usemi, "werevu mwingi huondoa maarifa".
Angaligawa mapato kwa ratili iliyopangwa awali
Na kwa kuheshimu kiu cha kambi yake na ya wenza,
Mti wa uelewano ungezidi kuzaa matunda matamu
Leo,kwa furaha, tungalikuwa tukiyala yakiwa mabivu.
(ub 1 wa "Werevu")

Badala ya kuongozwa na ndoto ya taifa angavu.
Mgavi alizingatia sauti laini za genge la walafi.
Akawapakulia thuluthi mbili za sinia la ngawira
Na kuwapunja simba waliopigana kwa meno na kucha.
(ub 2 wa "Werevu")

Pamoja na kiambishi nafsi **a** kupata fasiri katika ubeti wa pili, urudiaji wa kiambishi nafsi hiki na hali ya masharti **ngali** umejenga takriri katika ubeti huu. Beti hizi zimefumwa pamoja na urejelezi huu na kuwa matini moja.

Urejelezi wa kikatafora pia umetumika katika shairi la **Msimu wa Tisa.** Kiambishi nafsi **wa** ambacho kimetumiwa kuanzia ubeti wa tatu hadi mwisho wa shairi kimekuza taharuki katika shairi hili. Msomaji hajui wanaorejelewa kwa kiambishi nafsi hiki ni kina nani hadi anapofika mwisho wa shairi ndipo fasiri ya kiambishi hiki inaeleweka kurejelea **waheshimiwa** ambao tangu mwanzo hawatajwi. Kutokana na urejelezi huu, tunapata kujua tabia/sifa za **waheshimiwa**. Wahusika hawa wamesawiriwa kama wabinafsi,

wabadhirifu, wazembe na wasiowajibika. Urejelezi huu umechangia muumano katika shairi hili, had mwishoni mwa shairi fasiri ya kiambishi nafsi **wa** inapopatikana. Aidha, mtiririko wa shairi hili umetegemea urudiaji wa kiambishi nafsi **wa** ambacho kinapatikana katika beti nyingi na kuonyesha kuwa wazo moja linajitokeza katika beti hizi, hivyo kukuza uthabiti wa shairi kama ifuatavyo:

Waliovishwa makoja katika baraza la walaji wapya
Walipeperusha bendera kwenye mabenzi ya bei duwazi
(Ub. 4)
Walijinadi kwa akina yahe waliovaa matambara
Walitifua vumbi kwa mabenzi na mapajero mapya
( ub 5)
Wameshika rungu nzito ya kupiga dafrau bajeti ya taifa
Kwa ubinafsi usiojali walio kwenye minyororo ya ukame.
Wamejitwalia marupurupu laanifu eti ya kulipia usafiri
(ub. 6)
Wanalitimiza kwa kujikokota kama konokono au yungiyungi
Wamegeuza ukumbi wa taifa nembo ya uzembe na aibu. (ub. 7)

Karaha ya upungufu kwenye ukumbi wa *waheshimiwa!*
Inapoendelea kughasi hisia siku zilizofikia mwisho. (ub.12)

## 2.3 UDONDOSHAJI NA UBADILISHAJI

Uchanganuzi wa aina hizi mbili za muala umefanywa pamoja kwa sababu mbinu hizi zinarejelea wazo moja kwa vile katika ubadilishaji, kipashio kimoja huwachwa na badala yake kingine kutumiwa na katika udondoshaji kipashio kinadondoshwa na

kuwakilishwa kwa umbo kapa. Udondoshaji na ubadilishaji ni aina za muala ambazo hutumiwa ili kujiepusha na marudio yasiyofaa.

Shairi la "Nahodha na Jahazi" limeonyesha mfano mmoja wa udondoshaji:

Tungelikuwa kwenye ukungu wa jana
Tungesema mchawi mwenye stadi kuu
Ametuzinga kwa kipi cha mwewe
Au kwa meno ya ngiri na mkia wa kindi
(ub 1 wa "Nahodha na Jahazi")

Katika mshororo wa nne, neno **ametuzinga** limedondoshwa baada ya **au**. Huu ni udondoshaji wa kitenzi. Hata hivyo, maana ya mshororo huu bado inajitokeza bila utata wowote. Pengo lililoachwa linatuekeleza kutazama nyuma ya shairi kupata ufasiri wake, hivyo kufasiri ubeti huu kama matini moja. Mfano mwingine wa udondoshaji ni kama ufuatao:

Gari la siasa likaacha barabara ya lami
Na kujitosa kwenye ujia wenye udongo chepechepe
Mwendo wa kasi tuliotarajia utufikishe kwenye ufanisi
Ukawa safari ya kusukuma na kuvuta matopeni
Kusudi mgavi asukumiwe gari lipite kinamo lovulovu.
(ub 4 wa "Werevu")

Katika ubeti huu, udondoshaji wa nomino umetumiwa katika mshororo wa nne ambapo nomino **gari** imedondoshwa. Fasiri ya pengo hili inapatikana kwa kurejelea nyuma kwa nomino **gari** katika mshororo wa kwanza hivyo kudhihirisha uthabiti wa ubeti huu.

Ubadilishaji ni aina ya muala ambayo imetumiwa katika baadhi ya mashairi badala ya udondoshaji. Katika ubadilishaji neno la awali linadondolewa na badala yake lingine likatumika. Kwa mfano:

> Wakitishia polisi kwa mbwa wakali katika kasri zao
> Kijeuri, wakichomoa bastola dhidi ya wahudumu wa umma.
> (ub 7 wa "Tope la Mizozo")

Katika mishororo hii, maneno **wahudumu wa umma** yametumiwa kurejelea **polisi**. Fasiri inapatikana katika ubadilishaji huu kwa sababu nomino hizi zinahusu dhana moja hivyo kufasirika kama matini moja.

Katika ubeti wa mwisho wa shairi "Msimu wa Tisa", neno **wasaliti** limetumiwa badala ya **waheshimiwa.** Ubadilishaji huu ambao ni wa nomino umejenga muala kwa vile wazo ni lile tu. Nomino hizi zinarejelea wahusika wale wale tu, ila kwa sababu ya vitendo vyao viovu ndipo **waheshimiwa** hawastahili kupewa heshima yoyote na badala yake kurejelewa kama **wasaliti** kwa sababu ya kusaliti wananchi waliowachagua.

## 2.4 UUNGANISHAJI

Uunganishaji ni aina nyingine ya muala ambayo imetumika katika mashairi ya diwani ya *Msimu wa Tisa.* Muala umejengwa kutokana na maana inayobebwa na kiunganishi ambayo hudokeza kuwepo kwa faridi nyingine katika matini. Katika kufanya hivi, uunganishi huyaleta matukio ya matini pamoja na kuchangia kuibua maana.

Uunganishaji waweza kuwa baina ya neno, kishazi au sentensi. Viunganishi vya aina mbalimbali vimetumiwa katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.*

Matumizi ya kiunganishi **lakini** ambacho ni cha kinyume cha yale tunayatarajia yameonyesha tofauti za mitazamo. Mathalan:

> Ametuzinga kwa kipi cha mwewe
> Au kwa meno ya ngiri na mkia wa kindi
> Lakini leo jua la sayansi limemulika anga
> Linamwaga mwangaza wa ufahamu uani
>
> (ub 1 wa "Nahodha na Jahazi")

Katika ubeti huu, tofauti ya mitazamo inajitokeza kwa sababu zamani ushirikina uliaminiwa sana tofauti na enzi za leo ambapo sayansi imeleta mwangaza na kufanya watu kufahamu mambo. Tofauti hizi za mitazamo zimedhihirishwa na matumizi ya kiunganishi **lakini** ambacho kinajenga muala kwa kuunganisha matukio haya tofauti.

Uunganishaji umetumiwa katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* kuyahusisha matukio pamoja kwa kuonyesha mpito wa wakati. Kiunganishi **kisha** ambacho ni cha wakati kinaonyesha mfuatano wa matukio kiwakati na huelekeza msomaji kujua kuna tukio lililotangulia. Kwa kurejelea nyuma kuelewa tukio lililotajwa awali muala hujengwa. Matukio yanapounganishwa hukuza muumano wa shairi na kulifanya kufasiriwa kama matini moja. Mathalan:

Ichunguze kama njaa inaweza kuua

Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Ihariri taarifa ya tume ya rais.
(ub 1 wa "Tume za Rais")

Katika ubeti huu, kuna matukio mawili yanayotekelezwa na **tume ya rais**, matukio haya yanaonyesha wajibu wa kuchunguza na kuhariri kwa tume ya rais. Mfano mwingine:

Ichunguze jina la Rais wa Jamhuri,
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imtangazie Rais jina la Rais.
(ub 2 wa "Tume za Rais")

Katika ubeti huu, dhana ni moja inayolenga wajibu wa **tume ya rais** utakaotekelezwa baada ya mpito wa wakati. Mfano mwingine:

Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais.
(ub. 3 wa "Tume za Rais")

Ubeti huu unaeleza matukio mawili yakutekelezwa na tume. Tukio la kuchunguza na pili kushauri. Mfuatano wa matuko haya kiwakati umefanikishwa na matumizi ya kiunganishi **kisha.**

Uunganishaji ambao umetumika kwa wingi katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* ni ule wa kuongeza ambao huweka pamoja dhana mbili. Matumizi ya kiunganishi **na** humwelekeza msomaji kujua kuna wazo ambalo tayari limetajwa na bado kuna maongezi yanayofanywa. Mathalan:

> Wenye tamaa kubwa ya kuwapiku wengine
> Walitumia ujanja kwenye sinia ya mamlaka
> Wakajitwalia minofu na kuwachia wenzao makano
>
> (ub 3 wa "Tope la Mizozo")

Katika ubeti huu, kuna mawazo mawili yanayohusu sifa za wahusika ambao ni wanasiasa. Wazo la kwanza linahusu ulafi nalo la pili linahusu ubinafsi na yamefumwa pamoja na kiunganishi hiki. Mawazo yote mawili yanahusiana kwa vile yanaonyesha tabia za viongozi hawa. Mfano mwingine:

> Wahuni wa kigeni wamekaribishwa nchini kwa siri
> Na kupewa vyeo vikuu na funguo za milango ya chuma.
>
> (ub 7 wa "Tope la Mizozo")

Mishororo hii inadhihirisha mfumo wa ubeti huu ambao umetokana na matumizi ya kiunganishi **na** ambacho kimeleta pamoja dhana tofauti na kuzifuma kama kitu kimoja. Vitendo vya serikali vya kuonyesha ukarimu kwa **mamluki** vimefumwa pamoja na kufanya ubeti huu kuwa kitu kimoja. Tutazame mfano ufuatao:

Vitabu vya historia vitakapomlika msimu wa tisa
Vitatesa pua kwa harufu kali kama uzushi wa kicheche
Mnuko wa wasaliti waliovishwa magwada ya heshima
Na kulishwa mayai, maziwa, asali na nyama ya nundu
Kwa miaka mitano ya usaliti unaonguruma kama radi.
(ub 13 wa "Msimu wa Tisa")

Kiunganishi **na** kinafanya ubeti huu kufasirika kama matini moja kwa sababu ya wazo moja linalozungumziwa. Wazo hili linahusiana na matendo mazuri waliyofanyiwa waheshimiwa ili watekeleza wajibu wao lakini hawakuwajibika. Kiunganishi hiki kimetupa picha kamili ya kile kinachoelezwa na kufanya ubeti huu kuwa na muumano. Mfano ufuatao pia unaonyesha matumizi ya kiunganishi **na:**

Si ajabu walioliwa bangu na kuteswa na kuteswa na moto wa majuto
Walijiandaa na kusubiri kwenye medani ya mkataba mkuu
Punde viganja vilikazwa katika kamba ya "Vuta Tuvutane"
Vidole vya mguu vikajikita katika udongo mzito wa kinamo
Werevu wakaangushwa na kubururwa kwenye tope la aibu.
(ub 3 wa "Werevu")

Katika ubeti huu, matukio tofauti yameletwa pamoja kwa kutumia kiunganishi **na.** Dhuluma, tofauti pamoja na vitendo vya wadhulumiwa vimeunganishwa na kiunganishi **na**, hali ambayo imefanikisha kueleza yaliyomo.

Mfano mwingine:

Kwa kuogopa kutereza na kukwama kwenye mitaro,
Amelainisha makabila kwa mabenzi yenye bendera
Na kuongeza idadi ya wanaokamua nchi kwa fujo
Kinyume na ahadi iliyong'aa jana kama nyota.
(ub 5 wa "Werevu")

Katika ubeti huu, wazo la kwanza limefafanuliwa zaidi na wazo la pili kwa kutumia kiunganishi **na**. Kwa sababu ya kutotaka kuonekana kama walioshindwa na uongozi, viongozi hawa wanafuja mali ya umma wakitaka kuwafurahisha waliowachagua.

Matumizi ya kiunganishi **baada ya** hudhihirisha mfuatano wa matukio. Kiunganishi hiki huelekeza msomaji kujua kuna matukio mawili yanayohusiana. Matumizi ya kiunganishi hiki ni kwa kiasi kidogo katika mashairi ya *Msimu wa Tisa.* Mfano ni:

Baada ya kupingwa kutunyanganya mwishoni mwa msimu
Wameshika rungu nzito ya kupiga dafrau bajeti ya taifa.
( ub 6 wa "Msimu wa Tisa")

Mishororo hii imefumwa pamoja kuonyesha vitendo vya wanasiasa kama walafi kwa kutumia kiunganishi **baada ya.** Mfano mwingine:

Tukajijeruhi koo kwa kuimba "Juu! Juu! Juu sana!"
Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi.
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK 47
( ub 2 wa "Magenge Matatu")

Matukio katika ubeti huu yanahusiana na hurejelea uharibifu wa taifa uliosababishwa na viongozi wa kisiasa. Matukio haya yanatokea baada ya mpito wa wakati kama inavyoonyeshwa na kiunganishi **baada ya.**

## 2.5 MUALA WA KIMSAMIATI

Muala wa kimsamiati hutegemea uteuzi wa msamiati katika matini. Uteuzi huu waweza kuwa wa antonimu, sinonimu, hiponimu na hata maneno yanayohusiana. Aidha, muala wa kimsamiati huendelezwa na urudiaji ambao waweza kuwa wa neno, kirai au kishazi. Mbinu mojawapo ya wizani ambayo imetumiwa katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* ni usambamba.[1] Miundo tofauti ya maneno lakini inayorejelea wazo moja imetumiwa kujenga muumano katika mashairi haya Katika diwani hii uteuzi wa msamiati umechangia katika kuendeleza maudhui ya matini. Uteuzi wa msamiati licha ya kufanikisha muala wa matini umeleta mwendelezo wa dhana.

Muala wa kimsamiati katika matini hii umejidhihirisha kupitia kwa matumizi ya msamiati unaohusiana. Mathalan:

> <u>Nahodha</u> angelimakinika kwenye usukani
> Wasaidizi wake wangelidhibiti <u>matanga</u>
> <u>Jahazi</u> halingelidumu kwenye mlango wa <u>bahari</u>
> Likisukwasukwa na <u>mawimbi</u> yanayozozana
>
> (ub. 2 wa "Nahodha na Jahazi")

Katika ubeti huu, msamiati unaohusiana umechangia kukuza wazo linalozungumziwa. Nomino ambazo zimepigiwa msitari zimejenga muala kwa vile zinarejelea dhana ya

ushirikiano baina ya viongozi na wasaidizi wao katika kutekeleza kazi zao katika ulimwengu ulio na matatizo mengi. Tutazame mfano huu:

Zilifuata ziara za kubenua kifua na kuteuka vijijini
Walijinadi kwa akina yahe waliovaa matambara
Walitifua vumbi kwa mabenzi na mapajero mapya
(ub. 5 wa "Msimu wa Tisa")

Ubeti huu umedhihirisha muala wa kimsamiati. Nomino ambazo zimepigiwa mstari zinahusiana kwa vile ni msamiati unaohusu magari hasa ya watu wa vyeo vya juu. Msamiati huu umechangia kuonyesha hali ya maisha ya viongozi kutokana na magari wanayotumia. Mfano mwingine:

Waziri hayumo anacheza gofu na majambazi wa kigeni
Badala ya naibu wake kuwapo kujaza pengo la wizara
Yumo kitandani amelemazwa na manofu ya nyama ya jana
(ub. 11 wa "Msimu wa Tisa")

**Waziri** na **wizara** ni msamiati unaohusiana kwa vile unaonyesha mhusika na kazi anayotekeleza. Aidha, msamiati huu unahusiana na **mabenzi** na **mapajero** na unapatikana katika shairi moja, hivyo kukuza muumano wake na kuonyesha ni matini moja kwa sababu ni mawaziri ambao wanatumia magari ya aina hii ambayo wamepewa na serikali.

Shairi la " Msimu wa Tisa" lina matumizi ya sinonimu katika mfano huu:

Ni nani atakayeimba wimbo wa uzalendo
Katika huu ukumbi wa msimu laanifu wa tisa
Ambamo nyoyo za waliotumwa kujenga taifa
Zinadunda kwa mpigo wa binafsi uliokithiri
Ukumbi ambamo wingu la nzige wa jangwa
Linakula karamu haramu kwenye mti wa jamhuri
(ub. 2)
Punde walipokula kiapo cha uaminifu kwa nchi.
Bila kujali vinywa vinavyopiga miayo ya njaa
Walivamia ghala la taifa kwa tamaa inayovuma
(ub. 3)

Katika beti hizi, **taifa, jamhuri** na **nchi** ni sinonimu ambazo zinarejelea wazo moja na zimejenga muala. Nao msamiati wa **waziri** na **wizara** unahusiana na nomino hizi kwa sababu **waziri** hutekeleza kazi ya **wizara** ya **taifa/jamhuri**/au **nchi.** Msamiati huu wote unapatikana katika shairi moja hivyo kukuza uthabiti wake.

Matumizi ya msamiati unaohusiana pia yanapatikana katika mfano huu:

Mnuko wa wasaliti waliovishwa magwanda ya heshima
Na kulishwa mayai, maziwa, asali na nyama ya nundu
Kwa miaka mitano ya usaliti unaonguruma kama radi
(ub. 13 wa "Msimu wa Tisa")

Nomino ambazo zimepigiwa mstari zinahusiana na hukuza wazo moja linalohusu maisha mazuri ambayo viongozi huishi. Msamiati wa aina hii umefanikisha dhamira ya kuonyesha maisha ya starehe ya viongozi wa kisiasa.

Muala wa kimsamiati umechangia kuibua dhamira ya shairi la "Kitini".[2] Uteuzi wa msamiati unaolandana unadhihirisha kuwa wazo linalozungumziwa ni moja, hali inayofanya shairi hili kufasirika kama matini moja. Matumizi ya maneno kama vile: **waziri chama, siasa, mkombozi** na hata **taifa** yametuelekeza kujua kuwa wazo linalozungumziwa linahusiana na siasa.

Shairi la "Tume za Rais" limeonyesha matumizi mengi ya msamiati unaohusiana ambayo yamechangia katika kujenga taswira ya wazo linalozungumziwa. Uteuzi wa maneno kama vile : **hummer, rais, kasri, mkopo, akiba, mvinyo** na **sefu** ni mwafaka kwa sababu msamiati huu wote unahusiana na uluwa, cheo, na utukufu. Ujumbe ambao umeelezwa na uteuzi huu wa msamiati ni ubadhirifu wa mali ya umma unaofanywa kwa kushiriki katika vitendo vya utukufu. Katika kuoanisha msamiati na wazo linalozungumziwa, dhamira ya shairi imefanikishwa. Mathalan:

> Napendekeza tuuande tume ya rais
> Tumnunulie kila mwanatume <u>Hummer</u>
>
> (ub. 1)
>
> Napendekeza tuunde tume ya rais
> Tumjengee kila mwanatume <u>kasri</u>
>
> (Ub. 2)
>
> Napendekeza tuunde tume ya rais
> Tuitengee nusu ya <u>akiba</u> ya Banki kuu
>
> (Ub. 3)
>
> Napendekeza tuunde tume ya raisi
> Tuilipe kwa mkopo kutoka vitanzi vya Breton Woods
> Baada ya miaka mitano ya kumandari na kunywa <u>mvinyo</u>
>
> ("Tume za Rais")

Uteuzi wa msamiati mwafaka ambao umefungamana na muktadha umechangia kulipa shairi la "Magenge Matatu" uthabiti. Muala wa kimsamiati umejitokeza kupitia kwa matumizi ya msamiati unaohusiana. Mathalan:

Genge la kwanza la mazimwi
Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua maradhi na umaskini.
Tukanengukanenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele
Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi.
Ukazima mwenge wa utaifa na kuangusha uzalendo mtaroni.
Harufu ya ukabila ikachafua nchi kama uzushi wa kicheche.

(ub. 1)

Msamiati uliopigiwa mstari unaonyesha hali mbalimbali za maisha. **Kutojua, maradhi** na **umaskini** ni hali ya kusikitisha kwa vile ni kiwango cha chini cha maisha ambacho kina usumbufu mwingi. Ahadi zilizotolewa ili kutupilia mbali hali hizi ili kuwe na hali ya furaha ambayo imewakilishwa na msamiati wa **shangwe** na **vigelegele,** msamiati unaoeleza wazo moja. **Ulafi** na **ufisadi** ni msamiati unaolandana kwa vile **ufisadi** ni matokeo ya **ulafi,** hali ambayo ni ya kusikitisha kwa umma. Msamiati wa aina hii umejenga muala kwa sababu wazo linalohusu hali tofauti za maisha limeelezwa. Mfano mwingine:

Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya amani, upendo na umoja.
Tukajijeruhi koo kwa kuimba "Juu! Juu! Juu sana!".
Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi.
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK 47
Zao la umaskini unaovuma kama bahari kwenye miamba

Msamiati ambao unahusiana wa **amani, upendo** na **umoja** unakaribiana na umefanikisha kuonyesha picha kamili ya maisha mazuri ambayo yaliahidiwa na magenge lakini hayakutolewa. Aidha, hali ya uharibifu imesawiriwa na matumizi ya **viwavi** na **nzige**.

Genge la pili la mazimwi lilisababisha uharibifu mkubwa kwa nchi mithili ya viwavi n nzige. Ujumbe uliomo katika beti hizi unalenga kuonyesha kuwa badala ya maisha mazuri, wananchi walibakia kuishi maisha mabaya. Taswira hizi zenye ukinzani ambazo zimechangia kuibua maana ya shairi hili zimejitokeza kwa kutumia msamiati wa aina hii.

Mfano wa antonimu ambao umejenga muala wa kimsamiati ni huu:

Walitumia ujanja kwenye sinia ya mamlaka
Wakijitwalia <u>minofu</u> na kuwachia wenzao <u>makano</u>
(ub. 3 wa "Tope la Mizozo")

Katika ubeti huu neno, **minofu** linarejelea vyeo vya juu vinavyothaminiwa ilhali neno **makano** linarejelea vyeo vya chini. Antonimu hizi zimetumiwa kuonyesha wazo moja la ulafi/ubinafsi wa viongozi. Katika kutumia kinyume, wazo hili linasisitizwa.

Usambamba kama mbinu mojawapo ya kuwizani imetumika katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* kujenga muala. Tazama mfano huu:

Watakuja kutugawia peremende zenye sumu
Wataleweshа watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
(ub 1 wa "Msimu mwingine wa Wasaliti")

Mishororo hii mitatu imedhihirisha usambamba kwa sababu imebeba wazo moja ambalo ni unafiki wa viongozi wa kisiasa. Vitendo vyao vya kinafiki vimeelezwa kwa maneno tofauti. Aina hii ya muundo imetupa taswira nzuri ya wahusika hawa ambao wanagawia watu mazuri yenye madhara ya kupumbaza akili zao pamoja na kutoa ahadi nzuri ambazo

hawatimizi. Maneno tofauti yametumiwa kueleza wazo moja na kukuza uthabiti wa shairi hili. Mfano mwingine:

> Tulipoguna kwa maumivu makali kwenye misuli
> Juhudi za kizalendo zilipopamba moto yakini
> Tulipotokwa na michirizi ya jasho tukisaka utu
> Tulipopambana na dhiki ya giza la miongo miwili
> (ub 2 wa "Kitini")

Muala umejengwa na kufanya ubeti huu kuwa na muumano kwa vile wazo la ukombozi au kujitolea mhanga kupigania ukombozi ndilo linalotawala hivyo kufanya ubeti kuwa thabiti japo kuna matumizi ya msamiati tofauti.

Katika shairi la " Tume za Rais", mbinu ya usambamba imechangia pakubwa kutoa picha halisi ya wazo linalozungumziwa. Vitendo tofauti vya tume za rais vimeelezwa kwa maneno tofauti. Wazo kuu katika shairi hili ni ubadhirifu wa mali ya umma. Hii ni kwa sababu tume hizi haziwajibiki kwa vile hakuna ripoti zinazotolewa. Ufujaji wa mali ya umma na wanatume ni kwa wao kununuliwa 'hummer', kujengewa kasri, kutengewa nusu akiba ya Banki Kuu na hata kulipwa kwa mkopo. Beti zote za shairi hili zina muumano kwa kuendeleza wazo moja, hali inayofanya shairi hili kuwa matini thabiti.

Shairi la "Magenge Matatu" limetumia mbinu hii ya usambamba kwa sababu wazo linaloelezwa katika beti zote ni uongozi mbaya kwa vile viongozi hawatimizi ahadi wanazotoa.

Tazama mfano huu:

Genge la kwanza la mazimwi
Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua, maradhi na umaskini
Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi
Ukazima mwenge wa taifa na kuangusha uzalendo mtaroni
(ub 1)

Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya amani, upendo na umoja
Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK 47.
(ub 2)

Genge la tatu, nusu - mazimwi
Lilituahindi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
Baada ya miaka minne ya hila, tamaa, na uzingizi ulingoni
Imemezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi
(ub. 3)

Katika beti hizi, usambamba unajitokeza kwa ahadi zinazotolewa na matokeo ya kutotekeleza ahadi hizo.

## 2.6 MAJEDWALI YA VIPASHIO

Majedwali yafuatayo yanaonyesha vipashio mbalimbali katika kila shairi. Tumebainisha katika kila ubeti kipashio kinachosababisha muala, aina ya muala inayojitokeza na hatimaye kuonyesha kipashio kinachorejelewa.

**2.6.1 NAHODHA NA JAHAZI**

*(Msimu wa Tisa: ukurasa 5)*

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1 na 2 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 2 | mwenye | urejelezi | mchawi |
| | 3 | a- | urejelezi | mchawi |
| | 4 | ø | udondoshaji | ametuzinga |
| | 4 | au | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | na | uunganishaji | neno tangulizi |
| | 5 | lakini | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 5 | li- | urejelezi | jua |
| | 6 | li- | urejelezi | jua |
| 2 | 1 | a- | urejelezi | nahodha |
| | 1 | nahodha | msamiati | nahodha |
| | 2 | wake | urejelezi | nahodha |
| | 2 | wa- | urejelezi | wasaidizi |
| | 2 | matanga | msamiati | matanga |
| | 3 | jahazi | msamiati | jahazi |
| | 3 | li- | urejelezi | jahazi |
| | 3 | bahari | msamiati | bahari |
| | 4 | li- | urejelezi | jahazi |
| | 4 | na | uunganishaji | neno tangulizi |
| | 4 | ya- | urejelezi | mawimbi |
| | 4 | mawimbi | msamiati | mawimbi |
| 3 | 2 | u- | urejelezi | mkataba |
| | 2 na 3 | m- | urejelezi | nahodha |
| | 3 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 | ki- | urejelezi | kiti |
| | 4 | u- | urejelezi | mkataba |
| | 4 | na | unganishaji | kishazi tangulizi |
| 4 | 2 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 | zi- | urejelezi | hasira |
| | 3 | na | uunganishaji | kishazi tangulizi |
| | 3 | i- | urejelezi | mitingishano |
| | 5 | i- | urejelezi | mikono |
| | 5 | na | uunganishaji | kishazi tangulizi |
| 5 | 1 na 2 | u- | urejelezi | upepo |
| | 3 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | li- | urejelezi | taifa |

## 2.6.2 TOPE LA MIZOZO

*(Msimu wa Tisa: ukurasa 6-7)*

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1 na 2 | i-x3 | urejelezi | serikali |
| | 3 | a- | urejelezi | binadamu |
| | 3 | ki- | urejelezi | kiapo |
| | 5 na 6 | ni- | urejelezi | binadamu |
| 2. | 2 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 3 | wa- | urejelezi | viongozi |
| | 4 | li- | urejelezi | kapu |
| | 4 | u- | urejelezi | mchezo |
| 3 | 2 | wenye | urejelezi | werevu bila maarifa |
| | 3 na 4 | wa | urejelezi | viongozi |
| | 4 | na | uunganishaji | kishazi tangulizi |
| | 5 | u- | urejelezi | mkataba |
| | 6 | i- | urejelezi | gundi |
| 4 | 2 | i- | urejelezi | harufu |
| | 3 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | wa- | urejelezi | viongozi |
| 5. | 1 | ya | urejelezi | magari |
| | 3 na 4 | wa- | urejelezi | viongozi |
| | 4 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| 6. | 1 | wa- | urejelezi | viongozi |
| | 1 na 2 | wenye | urejelezi | wahuni |
| | 2 | i- | urejelezi | lugha |
| | 2 | wa- | urejelezi | samaki |
| | 3 | wale | urejelezi | viongozi |
| | 4 | wa- | urejelezi | viongozi |
| 7 | 1 | wahuni | msamiati | mamluki |
| | 1 | wa x 2 | urejelezi | wahuni |
| | 2 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 na 4 | wa - x3 | urejelezi | mamluki |
| | 3 | yenye | urejelezi | maneno |
| | 4 | wa- | urejelezi | mbwa |
| | 4 | zao | urejelezi | wahuni |
| | 5 | wa- | urejelezi | wahuni |
| | 5 | wahudumu wa umma | ubadilishaji | polisi |
| | 6 | wao | urejelezi | wahuni |
| | 6 | wenye | urejelezi | wafadhili |
| | 6 | ya- | urejelezi | mashagingi |
| | 7 | wa- | urejelezi | wafadhili |
| 8 | 1 | i- | urejelezi | misukumano |
| | 2 | m- | urejelezi | mwamuzi |
| | 2 | a- | urejelezi | mwamuzi |
| | 4 | i- | urejelezi | miguu ya taifa |

**2.6.3 WEREVU**

*(Msimu wa Tisa: uk 8)*

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1 | wa- | urejelezi | wajanja |
| | 2 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | i- | urejelezi | silaha |
| | 6 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 7 | i- | urejelezi | ratili |
| | 8 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 9 | u- | urejelezi | mti |
| | 9 | matamu | msamiati | matunda |
| | 10 | ya | urejelezi | matunda |
| | 10 | mabivu | msamiati | matunda |
| 2. | 2 na 3 | a- | urejelezi | mgavi |
| | 3 | wa- | urejelezi | genge la walafi |
| | 4 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | wa- | urejelezi | simba |
| 3. | 2 | na | uunganishaji | neno tangulizi |
| | 2 | wa- | urejelezi | walioteswa |
| | 2 | na | uunganishaji | neno tangulizi |
| | 3 | vi- | urejelezi | viganja |
| | 4 | vi- | urejelezi | vidole vya mguu |
| | 5 | wa- | urejelezi | werevu |
| | 5 | na | uunganishaji | kishazi tangulizi |
| 4 | 1 | li- | urejelezi | gari |
| | 2 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 2 | wenye | urejelezi | ujia |
| | 3 na 4 | u- | urejelezi | mwendo |
| | 4 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | ø | udondoshaji | gari |
| | 5 | a- | urejelezi | mgavi |
| | 5 | li- | urejelezi | gari |
| 5 | 1 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 2 | a- | urejelezi | mgavi |
| | 2 | yenye | urejelezi | mabenzi |
| | 3 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | i- | urejelezi | ahadi |

## 2.6.4 MSIMU WA TISA

(Ukurasa 9)

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | u- | urejelezi | ukumbi |
| | 2 | na | uunganishaji | neno tangulizi |
| | 3 | ki- | urejelezi | kimbunga |
| 2. | 3 | taifa | msamiati | taifa |
| | 4 | zi- | urejelezi | nyoyo |
| | 4 | u- | urejelezi | ubinafsi |
| | 6 | li- | urejelezi | wingu |
| | 6 | jamhuri | msamiati | taifa |
| 3 | 1 na 3 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| | 1 na 3 | nchi | msamiati | taifa |
| | 2 | vi- | urejelezi | vinywa |
| | 3 | i- | urejelezi | tamaa |
| 4 | 1 na 2 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| | 3 | zenye | urejelezi | ahadi |
| | 4 | i- | urejelezi | nidhamu |
| 5 | 2 na 3 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| | 2 | wa- | urejelezi | yahe |
| | 3 | mabenzi | msamiati | mabenzi |
| | 3 | mapajero | msamiati | mapajero |
| | 4 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| 6 | 1 | baada ya | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 | u- | urejelezi | ubinafsi |
| | 4 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| 7 | 1-4 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| 8 | 1 | vya | urejelezi | vikao |
| | 1 | vi- | urejelezi | vikao |
| | 3-5 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| 9 | 2 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| | 3 | baada ya | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | u- | urejelezi | uchaguzi |
| 10 | 1. | u- | urejelezi | muda |
| | 2 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| | 3 | a-x2 | urejelezi | muulizaji |
| | 3 | wake | urejelezi | muulizaji |
| | 4 | a- | urejelezi | muulizaji |
| 11 | 1 | li-x 2 | urejelezi | swali |
| | 3 | waziri | msamiati | waziri |
| | 3 | a- | urejelezi | waziri |
| | 4 | wake | urejelezi | waziri |
| | 4 | wizara | msamiati | wizara |
| | 5 | a- | urejelezi | naibu waziri |
| 12 | 1 | waheshimiwa | msamiati | waheshimiwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2 | i- | urejelezi | karaha |
| | 3 na 4 | wa- | urejelezi | waheshimiwa |
| | 5 | ya- | urejelezi | mabilioni |
| 13 | 1 na 2 | vi- | urejelezi | vitabu |
| | 3 | wasaliti | ubadilishaji | waheshimiwa |
| | 3 | wa- | urejelezi | wasaliti |
| | 4 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 5 | u- | urejelezi | usaliti |

## 2.6.5 MSIMU MWINGINE WA WASALITI

(Msimu wa Tisa: ukurasa 12)

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1 | wa- | urejelezi | vitambakwira |
| | 2 | zao | urejelezi | nyuso |
| | 3,4,5 | wa- | urejelezi | vitambakwira |
| | 3 | zenye | urejelezi | peremende |
| | 3 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 5 | yenye | urejelezi | kesho |
| | 5 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 5 | maziwa | msamiati | maziwa |
| | 5 | Asali | msamiati | asali |
| | 6 na 7 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 7 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 8 | wasaliti | msamiati | vitambakwira |

### 2.6.6 KITINI

*(Msimu wa Tisa: ukurasa 18)*

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1,3, na 4 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 2 | zi- | urejelezi | juhudi |
| | 5 | waziri | msamiati | waziri |
| | 5 | a-x2 | urejelezi | waziri |
| | 6 | zenu | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 6 | zenye | urejelezi | juhudi |
| | 6 | chama | msamiati | chama |
| | 7 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 8 | u- | urejelezi | wembe |
| 2. | 1,4,5 na 6 | a- | urejelezi | waziri |
| | 1 | chake | urejelezi | waziri |
| | 1 | ki- | urejelezi | chombo |
| | 2 | siasa | msamiati | siasa |
| | 2 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 | u- | urejelezi | ukweli |
| | 3 | m- | urejelezi | waziri |
| | 5 | u- | urejelezi | mwili |
| | 5 | mkombozi | msamiati | mkombozi |
| 3. | 1 | baada ya | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 1 | u- | urejelezi | umma |
| | 2 | wa- | urejelezi | umma |
| | 3 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 | i- | urejelezi | mikalatusi |
| | 4,5, na 6 | wa- | urejelezi | mawaziri |
| | 5 | taifa | msamiati | taifa |
| | 6 | u- | urejelezi | mti |
| | 6 | wa- | urejelezi | umma |

### 2.6.7 TUME ZA RAIS

*(Msimu wa Tisa: ukurasa 31)*

| **Ubeti** | **Mishororo** | **Kipashio cha muala** | **Aina ya muala** | **Kipashio kinachorejelewa** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 2 | m- | urejelezi | mwanatume |
| | 2 | hummer | msamiati | hummer |
| | 3 na 5 | i- | urejelezi | tume |
| | 3 | i- | urejelezi | njaa |
| | 4 | kisha | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | rais | msamiati | rais |
| 2. | 2 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 2 | m- | urejelezi | mwanatume |
| | 2 | kasri | msamiati | kasri |
| | 3 na 5 | i- | urejelezi | tume |
| | 4 | kisha | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| 3. | 2 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 2,3 na 5 | i- | urejelezi | tume |
| | 2 | akiba | msamiati | akiba |
| | 4 | kisha | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 5 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| 4. | 2 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 2 | i- | urejelezi | tume |
| | 2 | mkopo | msamiati | mkopo |
| | 2 | vya | urejelezi | vitanzi |
| | 3 | baada ya | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 3 | mvinyo | msamiati | mvinyo |
| | 4 | wa- | urejelezi | wanatume |
| | 5 | sefu | msamiati | sefu |
| | 5 | vya x 2 | urejelezi | vyumba |

### 2.6.8 MAGENGE MATATU

*(Msimu wa Tisa: Ukurasa 32)*

| Ubeti | Mshororo | Kipashio cha muala | Aina ya muala | Kipashio kinachorejelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | li- | urejelezi | genge |
| | 2 | maradhi | msamiati | maradhi |
| | 2 | maskini | msamiati | maskini |
| | 3 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 3 | shangwe | msamiati | shangwe |
| | 3 | vigelegele | msamiati | vegelegele |
| | 4 | ulafi | msamiati | ulafi |
| | 4 | ufisadi | msamiati | ufisadi |
| | 4 na 5 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 5 | u- | urejelezi | upepo |
| | 6 | i- | urejelezi | harufu |
| 2. | 2 | li- | urejelezi | genge |
| | 2 | amani | msamiati | amani |
| | 2 | upendo | msamiati | upendo |
| | 2 | umoja | msamiati | umoja |
| | 3 | tu- | urejelezi | mwandishi na wahusika |
| | 4 | viwavi | msamiati | viwavi |
| | 4 | nzige | msamiati | nzige |
| | 4 | wa- | urejelezi | viwavi na nzige |
| | 5 | jamhuri | msamiati | nchi |
| | 5 | i- | urejelezi | jamhuri |
| | 6 | u- | urejelezi | umaskini |
| 3. | 2 | li- | urejelezi | genge |
| | 2 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | baada ya | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 4 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |
| | 5 na 6 | i- | urejelezi | ahadi |
| | 6 | na | uunganishaji | sentensi tangulizi |

## 2.7 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeshughulikia vipengele vya muala ambavyo vinaifanya diwani ya *Msimu wa Tisa* kutambulika kama matini. Aidha, kwa kuchanganua diwani hii kimuala tumeweza kuonyesha jinsi maudhui yaliyomo yalivyowasilishwa. Aina zote za muala yaani urejelezi, ubadilishaji, udondoshaji, uunganishaji na muala wa kimsamiati zimechangia pakubwa katika kujenga maana za kisemantiki za mashairi ya diwani ya *Msimu wa Tisa.* Vipashio vya kisarufi na msamiati vimefumwa pamoja ili kuunda matini thabiti

Katika uchanganuzi huu, tumepata kuwa aina zote za muala zimetumiwa ingawa kwa viwango tofauti. Inadhihirika kuwa mbinu ya urejelezi imetumiwa kwa kiwango kikubwa katika mashairi yote. Hii ni kwa sababu kazi tulioshughulikia ni kazi ya fasihi andishi iliyo na maelezo ya matukio mbalimbali. Uhusiano uliopo baina ya matukio haya ni ule wa kurejelewa ambapo tukio moja hurejelea lingine katika kuibua maana.

Urejelezi ambao umetumiwa sana ni ule wa kiendofora ambao hutegemea muktadha wa kiisimu. Katika kutumia urejelezi wa aina hii, msomaji hupata maana halisi ya vipashio husika bila kupata shida ya kubainisha ni nini hasa kilichomaanishwa. Urejelezi wa kiendofora ambao umetumiwa sana katika mashairi haya ni wa kianafora ulio na matumizi mengi ya viambishi nafsi na vimilikishi. Viambishi hivi vimetumiwa kwa wingi ili kujiepusha na kurudiarudia wahusika na hali mbalimbali zilizomo kwenye matini. Aidha vitenzi vimetangulizwa na viambishi ambavyo huonyesha upatanishi wa kisarufi.

Muala wa kimsamiati na uunganishaji umetumiwa sana katika mashairi haya. Uteuzi wa msamiati umefanywa kimaksudi na umeoana na muktadha, hali ambayo imechangia pakubwa katika kueleza ujumbe uliokusudiwa.

Ubadilishaji na udondoshaji umetumiwa kwa kiwango cha chini sana. Hii ni kwa sababu aina hizi za muala hutumiwa ili kuzuia urudiaji usio na maana na hutumika sana katika matini zilizo ndefu. Mashairi aghalabu hutumia sentensi fupi fupi katika kueleza wazo fulani. Mashairi ambayo yamefanyiwa uchanganuzi yametumia sentensi fupi fupi na wala si marefu. Kwa mfano, shairi la ubeti mmoja halihitaji udondoshaji au ubadilishaji wowote. Ni kwa sababu ya mtindo huu wa ushairi ndipo aina hizi mbili za muala zimetumiwa kwa kiasi kidogo sana.

Ingawa viwango vya matumizi vimetofautiana, uchanganuzi huu umeonyesha kuwa kuna ugiligili mwingi baina ya aina za muala zilizotumiwa katika mashairi haya.

**TANBIHI**

1. Taz Wamitila. K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake,* Phoenix Publishers, Nairobi uk 102.
2. Taz Mberia K. (2007) *Msimu wa Tisa*, Marimba Publications Limited, Nairobi, uk 18.

# SURA YA TATU

# VIPENGELE VYA MSHIKAMANO KATIKA *MSIMU WA TISA*

## 3.1 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia mshikamano katika mashairi ya diwani ya *Msimu wa Tisa.* Nia yetu ni kubainisha vipengele vya mshikamano ambavyo vimechangia matini hii kuwa na muumano. Aidha, tunachunguza jinsi vipengele hivi vimechangia katika kuibua maana ya mashairi ya *Msimu wa Tisa.* Katika kufanya hivyo, uchanganuzi huu umejikita katika mwelekeo wa kinadharia wa umatini wa Beaugrande na Dressler (1981) unaosisitiza kuwa umatini haujengwi tu na muala pekee bali kuna kaida zingine za umatini.

Uchanganuzi wa mshikamano wa matini unategemea maarifa ya awali aliyonayo msomaji. Vile vile, ufasiri wa matini hutegemea muktadha wa kihali ambao huchangia katika kubainisha aina ya matini. Fasiri inayotolewa huwa inaingiliana na hali ya ulimwengu ilivyo. Kwa hali hii mshikamano, ni uchukulizi kuwa kinachosemwa au kinachoandikwa kitakuwa na maana kikihusishwa na maisha ya kila siku. Kama anavyosema Dijk (1977:4) matini iliyoshikamana hutarajiwa kusawiri mambo kama anavyotarajia msomaji ambaye hutoa fasiri ambazo zinaingiliana na visa ambavyo amevijua au amekumbana navyo. Hali hii hufanya mwingiliano wa matini kuwa sifa mojawapo ya kupima mshikamano wa matini.

Kwa kuchanganua diwani ya *Msimu wa Tisa,* tunatarajia itatimiza kaida za matini za aina yake. Mshikamano wa mashairi ya *Msimu wa Tisa* umepimwa kwa kushughulikia vipengele kama mpangilio wa sauti, maneno na mistari kwa kuchunguza jinsi mipangilio hii inavyokuza wizani ambayo ni sifa kuu ya mshikamano katika ushairi. Aidha, uchunguzi wa muktadha na mandhari pamoja na uhusiano wa anwani, mada na yaliyomo ni muhimu katika kudhihirisha mshikamano wa mashairi ya *Msimu wa Tisa* na kuifuma matini hii pamoja kama kitu kimoja.

## 3.2 MPANGILIO WA SAUTI

Ushairi hutumia mbinu ya takriri ambayo huwa na sauti moja au sauti tofauti bali za nasaba moja ya kifonolojia zinazorejelewa katika mshororo au mishororo kadha. "Katika kiwango cha sauti tunaona matumizi ya urudiaji katika takriri-irabu, takriri-konsonanti na kadhalika," Wamitila (2002: 107). Urudiaji huu wa sauti huimarisha wizani katika ushairi hivyo kujenga mshikamano katika shairi. Mashairi ya *Msimu wa Tisa* yana takriri-sauti inayojitokeza kwa mpangilio maalum. Sauti ambazo zimerudiwarudiwa zinapatikana mwanzoni mwa mshororo, hali inayosababishwa na idhini ya ushairi. Tazama mfano huu.

> <u>A</u>ngalipuuza mashauri ya wajanja waliomzunguka
> <u>Na</u> kuthamini maana ya maneno ya wimbo wa taifa
> <u>A</u>ngalizingatia kanuni za mkataba wa majemedari
> Silaha iliyokomboa taifa kutoka minyororo ya huzuni
> <u>A</u>ngalifahamu uaminifu ni akiba inayozaa matunda
> <u>Na</u> kukubali usemi: "werevu mwingi huondoa maarifa"
> <u>A</u>ngaligawa mapato kwa ratili iliyopangwa awali
> <u>Na</u> kwa kuheshimu kiu cha kambi yake na ya wenza (Werevu ub. 1 uk. 8)

Katika ubeti huu sauti **a** na **na** zimerudiwarudiwa na kuchangia kujenga mtiririko wa shairi. Wizani kama sifa ya mshikamano inajengwa na urudiaji huu ambao hutumiwa katika ushairi kwa kusisitiza wazo moja la uhusika na kufuma shairi pamoja kama matini moja.

Shairi la "kitini" pia lina mpangilio huu wa sauti ambapo ubeti wa kwanza una urudiaji wa sauti **tu** nao ubeti wa pili una urudiaji wa sauti **a** mwanzoni mwa mishororo. Msisitizo wa anayehusika unajitokeza kupitia kwa mpangilio huu wa sauti. Mfano mwingine wa takriri-sauti ni katika shairi la "Msimu Mwingine wa Wasaliti" ambapo mwanzo wa mishororo ya tatu, nne na tano kuna matumizi ya sauti **wa** iliyo na lengo la kusisitiza kama kaida ya ushairi. Msisitizo wa sauti **wa** ni kuonyesha hasa wanaohusika na wazo linaloelezwa hivyo kufuma shairi hili kama matini moja.

Katika shairi la "Tume za Rais", mpangilio wa sauti ni ule wa sauti **tu** kurudiwa mwanzoni mwa kila mshororo wa pili wa kila ubeti. Aidha sauti irabu **i** imetumiwa mwanzo mwa kila mshororo wa mwisho wa beti tatu za mwanzo. Pamoja na kusisitiza kile kinachohusika, sauti hii imechangia kukuza mtiririko wa shairi, na kuthibitisha kuwa kwa kuzingatia muktadha wa kihali takriri kama sifa mojawapo ya mashairi ya *Msimu wa Tisa* imekuza mshikamano.

Takriri – konsonanti pia imejenga wizani katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

Shairi la "Nahodha na Jahazi" ubeti wa tatu, sauti ya **k** imerudiwarudiwa katika mstari ufuatao:

Na kumkweza kwenye kiti kinachometameta

Shairi la "werevu" ubeti wa tano, konsonanti **k** imerudiwarudiwa katika mstari huu:

Kwa kuogopa kutereza na kukwama kwenye mitaro

"Msimu wa Tisa" ni shairi ambalo lina urudiaji wa konsonanti **m** katika mstari ufuatao:

Muulizaji hayumo miongoni mwa wachache ukumbini.

Mashairi ya *Msimu wa Tisa* yana mtiririko wa herufi zinazotoa sauti ya mlingamano zinazojitokeza katika uteuzi wa maneno. Ulingamano huu unapatikana katika mistari na kuendelea katika kila ubeti hivyo kufanya ubeti kujitosheleza. Ubeti unaojitosheleza huwa na muumano na kujidhihirisha kama ulio thabiti. Shairi ambalo halijajitosheleza katika beti zake hukosa mshikamano.

Shairi la 'Nahodha na Jahazi" lina mtiririko wa herufu zinazotoa sauti ya mlingamano kutokana na kuingiliana kwa herufi. Mfano huu unapatikana katika ubeti wa kwanza kama ifuatavyo:

Lakini leo jua la sayansi limemulika anga

Muungano wa herufi **l** na irabu tofauti tofauti umejenga wizani katika ubeti huu na kurahihisha matamshi ya mstari huu.

Shairi la "Msimu wa Tisa" katika ubeti wa tano lina sauti ya mlingamano kama ifuatavyo:

Kabla ya kuhama kama mbayumbayu wakati wa kiangazi

Konsonanti **k** pamoja na irabu tofauti zimekuza mtiririko wa ubeti huu.

Mifano zaidi ni:

Ubeti wa 11 wa "Msimu wa Tisa", mstari wenye mlingamano wa herufi ni ufuatao:

Swali la pili limeulizwa limechangamsha akili kwa ubora:

Takriri ya sauti **l** pamoja na irabu tofauti imefuma mstari huu pamoja.

"Msimu Mwingine wa Wasaliti" una mfano huu:

Vitambakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu.

Muungano wa herufi zilizopigiwa mstari umechangia katika kurahihisha matamshi ya mstari huu pamoja na kuchangia mtiririko wa shairi hili.

### 3.3 MPANGILIO WA MANENO

Mpangilio wa maneno hukuza wizani. Kama anavyosema Indangasi (1988:55) katika ushairi huru neno la mwisho katika kila mshororo huwa na mvuto wa kibinafsi pamoja na kuwa na shada. Hali hii hujenga wizani wa shairi na kufanya ushairi huru ambao hauzingatii urari wa vina kuwa na mshikamano. *Msimu wa Tisa* kama diwani ya ushairi huru haifuati kanuni ya mpangilio sawa wa vina bali hupata wizani kutoka kwa mpangilio wa maneno ya mwisho ya kila mshororo yenye shada.

Mshairi huwa na uhuru mkubwa katika matumizi ya lugha hali inayoathiri mpangilio wa maneno katika shairi. Katika *Msimu wa Tisa* kuna urudiaji wa maneno katika baadhi ya mashairi. Uamilifu wa urudiaji huu ni kusisitiza wazo linaloelezwa. Mathalan katika shairi la "Tume za Rais" neno **ichunguze** limerudiwa kwenye kila mshororo wa tatu wa beti tatu za mwanzo kuonyesha wajibu wa tume. Urudiaji kama sifa kuu ya ushairi

unadhihirisha mshikamano kwa kurejelea wazo moja katika shairi pamoja na kuwa mtindo unaochangia kujenga mtiririko wa shairi.

Katika shairi la “Magenge Matatu”, maneno **genge** na **mazimwi** yamerudiwa katika kila mshororo wa kwanza wa kila ubeti. Mpangilio huu wa maneno unadhihirisha kuwa wahusika wote wanaopatikana katika shairi hili wana sifa zao. Dhamira ya shairi ya kuonyesha kuwa hakuna tofauti kati ya viongozi wa nyakati hizi na wale wa zamani imefanikishwa na urudiaji wa haya maneno. Mshikamano wa shairi hili umekuzwa kwa mpangilio wa aina hii wa maneno ambao unafuma shairi nzima kama kitu kimoja kwa kuwa na wazo moja. Aidha, neno **lilituahidi** katika shairi la “Magenge Matatu” limerudiwa katika kila mwanzo wa mshororo wa pili katika shairi nzima. Urudiaji wa aina hii umejenga wizani wa shairi na kutambulisha shairi hili kama matini yenye mshikamano kama matini za aina yake pamoja na kufanikisha msisitizo wa wazo linaloelezwa la ahadi za uwongo.

Ukiushi wa kisemantiki unaopatikana katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* umesababishwa na mpangilio wa maneno kwa vile kuna baadhi ya maneno ambayo yametumiwa kwa maana tofauti na ile ya kawaida. Maneno kama haya yanapatikana katika shairi la “Werevu” lililo na mhusika anayejiona ni **mwerevu** na kupuuza sheria za uongozi na kanuni za mkataba na kufuata mashauri ya wajanja. Vitendo vyake havionyeshi uerevu wowote kwa sababu hatimaye anakumbwa na matatizo mengi katika utawala wake. Kwa kutumia ukiushi huu, shairi linaonyesha muumano uliopo kati ya anwani, dhamira na yaliyomo.

Ukiushi mwingine wa kisemantiki ni katika shairi la "Msimu wa Tisa". Neno **waheshimiwa** limetumiwa kwa ukinzani kwa sababu vitendo vinavyoelezwa vya wahusika havistahili sifa hiyo. Hatimaye wanasawiriwa kama wasaliti. Ukiushi wa aina hii unadhihirisha mshikamano katika shairi kwa sababu yaliyomo na wahusika yamejitokeza kama kitu kimoja.

## 3.4 MPANGILIO WA SENTENSI

Mashairi ya *Msimu wa Tisa* yana mipangilio tofauti ya sentensi. Baadhi ya mashairi yana urudiaji wa sentensi katika kila ubeti ilhali mengine hayana urudiaji wowote wa sentensi. Katika shairi la "Tume za Rais", sentensi ya kwanza katika ubeti wa kwanza imerudiwa katika mwanzo wa beti zingine nayo ni, **napendekeza tuunde tume ya rais.** Kwa kurudia sentensi hii, dhamira ya shairi hili hujitokeza kuwa uundaji wa tume za rais huwa ni kitendo kinachosisitizwa sana. Aidha, sentensi **kisha tuunde tume nyingine ya rais** imerudiwa katika kila mshororo wa nne wa kila ubeti. Urudiaji huu pia ni msisitizo wa uundaji wa tume za rais. Muundo huu wa sentensi unaofanana umejenga usambamba wa kisintaksia kwa sababu beti zote nne zinarejelea wazo lile lile hivyo kukuza mshikmano wa shairi. Ingawa kuna sentensi zingine tofauti ambazo zimetumiwa lakini muundo ni ule ule. Wazo kuu katika mpangilio huu wa sentensi ni kuonyesha kuwa tume za rais zinaundwa kila wakati. Urudiaji wa sentensi hizi mbili umekuza wizani katika shairi na kuonyesha uhusiano uliopo baina ya dhamira ya shairi na yaliyomo.

Shairi la "Magenge Matatu" pia lina matumizi ya usambamba wa kisemantiki, kwa vile shairi limetumia maneno tofauti lakini muundo ni ule ule. Muundo wa aina hii umeonyesha mshikamano katika shairi hili kwa kudhihirisha dhamira ya shairi kwa kutumia msisitizo wa maneno tofauti. Wazo kuu katika shairi hili ni kuonyesha utawala mpya katika enzi tofauti. Usambamba huu umesawiri enzi tofauti za utawala lakini mbinu mbaya za utawala ndizo zinazotumiwa.

Katika kuchunguza mpangilio wa sentensi katika "Msimu wa Tisa" ukiushi wa kisarufi umejitokeza kwa sababu kuna matumizi ya sentensi ambazo hazijakamilika bali zinaendelea kwenye sentensi zinazofuata. Mpangilio huu wa sentensi huonyesha mfululizo wa mawazo ambao hufika kikomo mwishoni mwa ubeti, sentensi inapokamilika na kuwa na mshikamano wa mada yaliyomo. Ukiushi huu wa kisarufi umesababisha mashairi yenye idadi tofauti ya mishororo na beti.

Mathalan, shairi la "Msimu Mwingine wa Wasaliti" lina ubeti mmoja wenye mishororo nane. Mawazo yote yameelezwa kikamilifu kwa ubeti mmoja ilhali shairi la "Msimu wa Tisa" lina beti kumi na tatu na kila ubeti una idadi tofauti ya mishororo. Wazo katika kila ubeti limefululizwa kwa idadi tofauti ya mishororo tofauti hadi kukamilika na kuibua maana. Mfano mwingine ni shairi la "Nahodha na Jahazi" lenye lenye beti tano zenye idadi tofauti za mishororo nalo shairi la "Tope la Mizozo" lina beti nane zenye idadi mbalimbali ya mishororo.

Mashairi ya *Msimu wa Tisa* yana mshikamano kama matini za aina yake kwa sababu ya mpangilio huu wa sentensi ambao humpa mtunzi uhuru wa kutozingatia idadi maalum ya beti na mishororo. Hata hivyo, diwani hii kama kazi ya kifasihi ya utanzu wake imetimiza kaida ya kuwa na mizani, mishororo na beti kama muundo wa kuelezea yaliyomo.

## 3.5 UHUSIANO WA ANWANI, MADA NA YALIYOMO

Mshikamano katika kazi ya kifasihi hupimwa kutokana na jinsi mwandishi anavyofungamanisha anwani, mada pamoja na yaliyomo ili kufanikisha dhamira ya matini. Kwa matini kutimiza kaida ya ukubalifu, lazima mada na yaliyomo yafungamane na anwani ya matini husika. Maelezo yanayotolewa kwenye matini lazima yahusiane na mada ili kuibua maana. Matini isiyofuata kaida hii hukosa mshikamano kwa sababu haijaibua maana inayodokezwa na anwani yake. Anwani za mashairi ya *Msimu wa Tisa* zinaoana na yaliyomo. Maelezo ambayo yametolewa katika kila shairi ni ufafanuzi mwafaka wa anwani ya shairi husika. Mathalan shairi la “Tume za Rais” limeelezea juu ya tume mbalimbali za rais zinazoundwa lakini hazitekelezi wajibu wao. Matokeo ya kuunda tume hizi yameelezwa na yanaonyesha hasara nyingi inayosababishwa na tume hizi.

“Msimu Mwingine wa Wasaliti” ni anwani ambayo inaoana ya mada na yaliyomo kwenye shairi. Viongozi wa kisiasa wanaochaguliwa ni sawa na wale waliotangulia kuongoza kwa vile wanatenda makosa sawa na waliowatangulia kuongoza. Aidha, ni

wasaliti kwa vile hawatimizi ahadi wanazotoa. Hila zao ndizo zinazowaduwaza wananchi na kuwafanya kurudia kosa kwa kuwachagua tena.

Mada inapofungamana na dhamira ya matini hufanikisha mshikamano kwa kuibua maana inayokusudiwa. Shairi la "Magenge Matatu" lina anwani inayofungamana na ujumbe uliolengwa. Shairi linaeleza juu ya enzi tatu tofauti za utawala, ambazo zina viongozi tofauti wanaotumia mbinu tofauti za utawala lakini matokeo ya utawala wao yanafanana kwa vile ni hali ya uharibifu inayosalia baada ya kila enzi ya utawala. Dhamira ya shairi hili ni kuonyesha kuwa viongozi wote ni sawa na kama magenge na mazimwi, kazi yao ni kubomoa kuliko kujenga nchi.

Maarifa ya awali yanachangia kufanikisha mshikamano wa anwani ya "Msimu wa Tisa" na mada. Shairi hili linaeleza vitendo mbalimbali vya waheshimiwa kwa muda wa miaka mitano waliochaguliwa. Vitendo vya wanasiasa pindi tu wanapoapishwa hadi wakati wao wa kuhudumu unapoisha vimesawiriwa kuwa vya kujitakia makuu pamoja na kutowajibika kikazi. Kwa miaka mitano waliochaguliwa, 'waheshimiwa' hawa wamesababisha hasara nyingi kwa nchi kama inavyoonekana katika ubeti wa mwisho uk. 11.

> Vitabu vya historia vitakapomlika msimu wa tisa
> Vitatesa pua kwa harufu kali kama uzushi wa kicheche
> Mnuko wa wasaliti waliovishwa magwanda ya heshima
> Na kulishwa mayai, maziwa, asali na nyama ya nundu
> Kwa miaka mitano ya usaliti unaonguruma kama radi

Ubeti huu unaonyesha uharibifu mwingi uliotekelezwa wakati wa msimu wa tisa. Vitendo vyote vya ulafi, ubinafsi, tamaa, ubadhirifu wa mali ya umma pamoja na uzembe na kutowajibika vinajitokeza katika shairi la "Msimu wa Tisa".

"Tope la Mizozo" ni anwani ambayo ni muhtasari wa yaliyomo kwenye shairi hili hali inayojenga mshikamano wa shairi. Anwani inahusiana na maudhui na dhamira ya shairi hili. Mzozo wa kwanza ni kati ya wanasiasa waliochaguliwa na wananchi unaosababishwa na viongozi kutotimiza matarajio ya wananchi. Mzozo wa pili ni kati ya wanasiasa wenyewe kwa sababu ya ulafi na ubinafsi wa baadhi yao, hivyo hawawezi kutangamana. Nao mzozo wa mwisho ni kati ya wahuni wa kigeni na wananchi, mzozo huu umesababishwa na tabia mbovu za wahuni hawa. Kwa kutupa taswira ya hali ya jamii hii, mshikamano wa anwani, mada na yaliyomo umefanikishwa.

## 3.6 MUKTADHA NA MANDHARI

Maana ya matini hutegemea maarifa ya kimuktadha aliyonayo msomaji, Blakemore (1987:109). Muktadha hujitokeza wazi kupitia uteuzi wa msamiati. Msamiati unaofungamana na muktadha huchangia kujenga mshikamano. Blakemore (1987:109) anaeleza kuwa muktadha huzua matarajio fulani kwa msomaji kuhusiana na yaliyomo katika matini.

Msamiati huchangia mshikamano kwa vile kila muktadha huwa na msamiati wake maalum. Msamiati unaohusiana na muktadha huibua maana ya matini kwa vile ni kupitia kwa muktadha ambapo mwandishi huteua msamiati kuwasilisha yaliyomo.

Msamiati ambao umeteuliwa kutumika katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* unaoana na muktadha wa kisiasa wa mashairi haya. Kwa mfano maneno kama vile: uzalendo, mkataba, mamlaka, siasa, uchaguzi, waziri, wizara, chama n.k. yametumiwa kuafikiana na dhana inayowakilishwa.

Kwa kiasi kikubwa, lugha ya matini ni lugha ya kipindi kilichoandikiwa ili kubainisha mandhari yake. Muktadha ambamo kazi ya kisanaa imezalika na mandhari ya kijiografia huchukuliwa kuwa muhimu mno. Mandhari hudhamiriwa kuzua maana fulani inayolingana na dhamira ya matini. Aidha "mandhari huathiri sana mkondo wa kimaudhui na huwa na athari kubwa kwenye dhamira kuu katika kazi inayohusika," Wamitila (2002:28)

*Msimu wa Tisa* ni diwani ambayo imeshikamana kama kazi ya kipindi chake kwa sababu msamiati uliotumiwa katika mashairi haya unaoana na utawala wa mwafrika baada ya uhuru. Kwa mfano, shairi la "Msimu wa Tisa" linaeleza juu ya vitendo vya **waheshimiwa** waliochaguliwa katika msimu wa tisa. Uchaguzi huu ulifanywa baada ya uhuru. Wahusika waliomo katika shairi la "Tope la Mzozo" ni thibitisho kuwa kipindi cha tawala katika "Msimu wa Tisa" ni baada ya uhuru. Muktadha wa kihali umechangia wazo hili kwa sababu katika shairi la "Tope la Mizozo" wahuni wa kigeni waliokaribishwa nchini kwa siri na kuvuruga usalama walifanya hivyo katika enzi ya utawala wa Mwafrika.

Mshikamano hujengwa na muktadha wa kihali. Mashairi ya *Msimu wa Tisa* yamesawiri utawala ambao una matatizo mengi kama vile: ufisadi, tamaa, ubinafsi, ubadhirifu wa mali ya umma, utowajibikaji n.k. Haya ni matatizo ambayo yalikumba nchi nyingi zinazoendelea baada ya kujinyakulia uhuru.

Shairi la "Tume za Rais" linathibitisha kipindi cha utawala wa Mwafrika baada ya uhuru. Hii ni kwa sababu huu ndio ulikuwa wakati miradi mingi ilianzishwa katika nchi zinazoendelea baada ya kujinyakulia uhuru lakini hazikutimilika. Uundaji wa tume kila baada ya nyingine una uhusiano mkubwa na kipindi kilichoandikia *Msimu wa Tisa.*

Katika shairi la "Magenge Matatu" mwandishi ametumia mandhari kihisishi kwa sababu mandhari haya yanaibua hisia za uchukivu na kukerwa kutokana na taswira ya viongozi wa kisiasa kuendelea kuzorotesha nchi yao kwa vitendo vya ufisadi na ubinafsi badala ya kutimiza ahadi walizotoa. Maudhui ya kuzoroteka kwa nchi yanaendelezwa na mandhari ya ulafi, ufisadi, tamaa, uharibifu, uzembe n.k. Mandhari haya yanawiana na wazo ambalo linaendelezwa kuwa viongozi wote wanafanana na mbinu zao tofauti za kutawala ni za kubomoa nchi. Hali hii imefanikisha dhamira ya shairi hili na kukuza mshikamano.

Mandhari yanakuwa muhimu kutokana na mchango wake katika kuwapa wahusika wasifu fulani. Hii inamaanisha kuwa tabia ya mhusika wakati mwingine hutegemea mazingira yanayomzunguka. Mashairi ya *Msimu wa Tisa* yamehusishwa na mazingira ya kisiasa. Siasa huhusishwa na ubinafsi, unafiki pamoja na kutokuwa na msimamo. Hali hii imedhihirishwa vizuri katika shairi la "Kitini" na waziri. Wazo lililokusudiwa

kuwasilishwa linahusu tabia za wanasiasa hasa wanapotaka kuibuka washindi. Watatumia kila hila ili kufaulu.

Katika shairi la "Werevu" tabia za viongozi wa kisiasa wanaochaguliwa zinajitokeza kupitia kwa mandhari iliyochorwa. Viongozi hawa wanasifika kwa kujifanya werevu lakini matokeo ya maarifa yao ni ya kuangamiza nchi. Sifa nyingine kama vile ulafi, ufisadi, na upuuzaji zinajitokeza kupitia kwa mandhari ambayo yamejenga mshikamano wa shairi hili kwa vile matini inasawiri mandhari tunayotarajia kukumbana nayo kutokana na uongozi wa aina hii.

### 3.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumechanganua vipengele vya mshikamano ambavyo vimechangia kujenga uthabiti wa mashairi ya *Msimu wa Tisa* kama matini. Diwani hii imezingatia kaida za lugha ya Kiswahili sanifu katika kutekeleza uamilifu wake kama kazi ya kifasihi. Katika kuibua maana, dhamira ya matini hii ya kusawiri jamii kisiasa imetimizwa kwa sababu ya mshikamano wa dhana zilizomo.

*Msimu wa Tisa* ni diwani ambayo imefuata kaida za utunzi wa matini ya aina yake kwa vile ina mtindo unaofungamana na matini nyingine za utanzu wake. Muktadha wa kihali umethibitisha kuwa mbinu ya usambamba wa sauti, maneno na sentensi ndiyo imetumiwa sana katika kujenga wizani ambayo ni sifa ya mshikamano wa mashairi.

Mshikamano katika mashairi ya *Msimu wa Tisa* umechangia kujenga vipengele vingine vya matini. Dhamira ya matini hii ni kuonyesha hali ilivyo katika mazingira ya kisiasa hasa katika nchi zinazoendelea. Masuala mbalimbali ya kijamii yamejitokeza kama vile ufisadi, ubinafsi, ubadhirifu, tamaa n.k Mshikamano wa yaliyomo na mtindo uliotumiwa kuyawasilisha umechangia kuibua maana ya mashairi haya na kufanya diwani hii kukubalika kama matini. Sifa ya mwingiliano matini imekuzwa na mtindo wa ushairi huru ambao umetumiwa katika kueleza masuala ya kijamii. Mshikamano wa yaliyomo na namna ambavyo yamewasilishwa umechangia katika kujenga uthabiti wa mashairi ya *Msimu wa Tisa.*

# SURA YA NNE

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 HITIMISHO

Katika tasnifu hii, tumechanganua muala na mshikamano katika mashairi ya diwani ya *Msimu wa Tisa*. Tumefanya hivyo kwa kutumia nadharia ya muala kama ilivyo pendekezwa na Halliday na Hasan (1976) pamoja na mtazamo wa umatini wa Beaugrande na Dressler (1981). Mwelekeo huu umetuwezesha kuichunguza matini kama yenye uamilifu wa kisarufi na jukumu la kijamii.

Katika utafiti huu, tumechunguza aina mbalimbali za muala pamoja na vipengele vya mshikamano vinavyojenga umatini katika maishari ya *Msimu wa Tisa*. Muala na mshikamano ndizo sifa za kimsingi za umatini zinazoyaunga maishairi ya diwani ya *Msimu wa Tisa* pamoja na kuyapa maana na uthabiti.

Katika utafiti huu, tumechunguza kwa undani muala unaotokana na urejelezi, ubadilishaji, udondoshaji, uunganishaji na muala wa kimsamiati. Utafiti huu umebainisha kuwa katika mashairi ya *Msimu wa Tisa*, kuna matumizi ya mbinu zote za muala. Hata hivyo, mbinu ya urejelezi imetumika zaidi kuliko hizo zingine. Hili linatosheleza makisio yetu kuwa baadhi ya vipengele vya muala vinatoa mchango mkubwa kuliko vingine katika kujenga umatini katika mashairi ya *Msimu wa Tisa*. Urejelezi wa kiendofora ndio uliotumiwa sana.

Madhumuni ya kuchunguza aina za muala ambazo zimetumiwa kwa wingi na zile ambazo zimetumiwa kwa kiasi kidogo yametimilika kwa sababu utafiti huu umebainisha kuwa urejelezi umetumiwa sana ilhali ubadilishaji na udondoshaji ndizo mbinu ambazo zimetumiwa kwa kiasi kidogo katika mashairi ya *Msimu wa Tisa*. Hii ni kwa sababu mbinu hizi hutumika sana katika mazungumzo ambapo mzungumzaji na msikilizaji huwa katika mazingira sawa na huweza kuelewana lakini kwa vile hii ni matini andishi, matumizi mengi ya udondoshaji na ubadilishaji huweza kuzua utata na kupotosha maana iliyokusudiwa.

Muala wa kimsamiati na uunganishaji ni mbinu ambazo zimetumiwa kwa ufanifu mkubwa na zimejenga umatini wa mashairi ya *Msimu wa Tisa*. Mashairi haya yametumia aina mbali mbali ya viunganishi ambavyo vimechangia kujenga umatini. Aidha, utafiti huu umethibitisha kuwa mbinu hizi za muala hutegemeana katika kuibua maana ya mashairi katika diwani hii. Uchanganuzi wa kimuala umebainisha diwani ya *Msimu wa Tisa* kama kipashio kilichozalika katika muktadha wa kiisimu na wa kihali.

Katika kutathmini mshikamano wa mashairi ya *Msimu wa Tisa* utafiti huu umechunguza mchango wa vipengele mbalimbali vya mshikamano kama vile: mpangilio wa sauti, maneno na mistari, uhusiano kati ya anwani, mada na yaliyomo pamoja na umuhimu wa muktadha na mandhari katika kujenga umatini. Uchanganuzi huu umebainisha kuwa mashairi ya *Msimu wa Tisa* yamejengeka katika muktadha wa kiisimu na wa kihali. Mshikamano wa matini waweza kupimwa kwa kuichunguza matini katika upekee wake ama kwa kuilinganisha matini husika na matini za aina yake.

Utafiti huu umechanganua mashairi ya *Msimu wa Tisa* kama matini ya utanzu wa kifasihi na kubainisha kuwa vipengele hivi ambavyo tumetaja vimechangia mshikamano kimaudhui, kimaana na hata kimtindo. Kwa kulinganisha *Msimu wa Tisa* na matini za utanzu wa ushairi inabainika kuwa mpangilio wa sauti, maneno na sentensi umejenga wizani ambayo ni sifa ya mshikamano katika ushairi. Nao uhusiano wa mada, anwani, yaliyomo muktadha na mandhari umechangia pakubwa katika kuibua maana ya mashairi kwa kuonyesha maudhui yaliyomo. Licha ya kuzingatia kaida za lugha ya Kiswahili sanifu, *Msimu wa Tisa* ni matini ambayo imetimiza majukumu yake kama kazi ya kifasihi na ya kijamii. Kama zao la jamii, diwani hii inamulika masuala ya kijamii ya wakati wake, hivyo kukubalika kama matini ya jamii-lugha yake.

Uchanganuzi wa kiisimu – matini tuliofanya pia umethibitisha ukweli wa nadharia tete kuwa muala na mshikamano ni sifa ambazo zimechangia kuwasilisha maudhui katika mashairi ya *Msimu wa Tisa*. Mbinu za muala ambazo zimetumiwa zimechangia katika kupata fasiri ya maana iliyokusudiwa katika kila shairi na hivyo kufanikisha uwasilishaji wa maudhui ya mashairi hayo. Aidha, uhusiano wa anwani, mada na yaliyomo umechangia pakubwa katika kudhihirisha masuala ya kijamii yaliyomo. Kutokana na vipengele vilivyochunguzwa, imebainika kuwa muala na mshikamano ni sifa ambazo zinathibitisha mashairi ya *Msimu wa Tisa* kama matini inayokubalika.

Nadharia ya muala kama ilivyopendekeza na Halliday na Hasan (1976) huzingatia muala kama sifa ya pekee ya kujenga umatini. Hata hivyo, uchunguzi huu umethibitisha kuwa umatini hujengwa na muala pamoja na sifa zingine kama vile: mshikamano, dhamira,

ukubalifu, kiasi cha yaliyomo, mahusiano na mwingiliano wa matini kama ilivyopendekezwa na Beaugrande na Dressler (1981).

Utafiti huu umetumia nadharia ya muala ambayo ina mbinu za ubadilishaji na udondoshaji zinazozuia urudiaji usiofaa. Mbinu hizi zinapatikana sana katika maandishi ya usimulizi lakini matini za kishairi ambazo huwa na mtindo wa lugha ya mkato na sentensi fupifupi, matumizi ya ubadilishaji na udondoshaji ni ya kiasi kidogo sana. Hizi ni mbinu zinazojitokeza sana katika matini ndefu ndipo matumizi ya nadharia ya muala yafanikiwe.

Aidha, nadharia ya muala hupendekeza matumizi ya urejelezi wa ekisofora katika matini. Maana iliyokusudiwa katika matini andishi hupatikana kwa kurejelea vipashio vya ndani. Matumizi ya ekisofora huweza kupotosha maana iliyokusudiwa hivyo kusababisha ukosefu wa umatini.

Muala wa kimsamiati huendelezwa kwa msamiati wa aina mbalimbali. Ingawa mashairi ya *Msimu wa Tisa* yana matumizi ya muala wa kimsamiati, msamiati uliotumiwa sana ni ule unaohusiana, kuna ukosefu wa matumizi ya hiponimu na mfano moja tu wa sinonimu na antonimu. Ili kuonyesha mchango wa muala wa kimsamiati kwa ufanifu, mashairi ya *Msimu wa Tisa* yafaa yawe na matumizi ya aina mbalimbali ya muala wa kimsamiati.

## 4.2 MAPENDEKEZO

Tasnifu hii imechunguza namna ya kutathmini mashairi ya *Msimu wa Tisa* kama matini. Uchanganuzi wetu umeshughulikia sifa mbili za matini. Tunapendekeza tahakiki za baadaye kufanya uchanganuzi wa kiisimu – matini wa ushairi huru zikitumia sifa zingine za umatini kama ilivyopendekewa na Beaugrande na Dressler (1981) nazo ni: dhamira, kiasi cha yaliyomo, ukubalifu, mahusiano na mwingiliano wa kimatini.

Ushairi huru unatofautiana na ushairi wa kimapokeo kimuundo. Tunapendekeza watafiti wa baadaye wafanye uchanganuzi wa kiisimu – matini wa mashairi ya kimapokeo ili kubainisha kama kuna tofauti za matumizi ya vipengele vya sifa za umatini. Aidha, tafiti za baadaye zaweza kufanya uchanganuzi wa kiisimu – matini kwa kulinganisha na kutofautisha mashairi huru na mashairi mapokeo.

Tumefanya uchanganuzi wa kiisimu – matini wa ushairi huru. Kuna haja ya uchanganuzi wa aina hii katika tanzu zingine za fasihi kama vile: tamthilia, hadithi fupi n.k. kwa kufuatia mtazamo huu wa kinadharia.

## MAREJELEO


Arege, T (1998) Ushairi huru wa Kiswahili: Mchango wa kezilahabi E. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Beaugrande, R na Dressler, W. (1981) *Introduction to Text Linguistics.* London, Longman.

Blakemore, D (1987) *Semantic Constraints on Relevance*. NewYork, Basil Blackwell Ltd.

Brown, G na Yule G (1983) *Discourse Analysis*. NewYork, Cambridge University Press.

Chiraghdin, S (1977) *Malenga wa Mrima.* Dar-es-Salaam, Oxford University Press.

Crystal, D (1997) *The Cambridge Encyclopedia of Language.* 2nd Edition, New York.

Dijk, V (1977) *Text and Context*. New York, Longman.

Habwe, J na Karanja, P (2004) Misingi *ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi, Phoenix Publishers.

Habwe, J. (1999) Discourse Analysis of Kiswahili Political Speeches. Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

Halliday, M na Hasan (1976) *Cohesion in English*. London, Longman.

Indangasi, H. (1988) Stylistics (Literature Part II) Mhadhara wa fasihi ya Kiingereza, Nairobi University Press.

Kahigi K, na Mulokozi, M (1979) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar-es-salaam. Tanzania Publishing House.

____________(1973) *Mashairi ya Kisasa*. Dar-es-Salaam, Tanzania Publishing House.

Kezilahabi, E (1974) *Kichomi.* Nairobi, Heinemann.

____________ (1988) *Karibu Ndani*. Dar-es-Salaam, Dar-es-Salaam University Press.

Leech, G na Short, M (1981) *Style in Fiction.* NewYork, London.

Mazrui, A (1988) *Chembe cha Moyo*. Nairobi, Heinemann.

Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi, Standard Graphics.

Mberia, K (1997) *Mchezo wa Karata.* Nairobi, Marimba Publications.

___________ (2001) *Bara Jingine*, Nairobi, Marimba Publications.

____________ (2007) *Msimu wa Tisa*. Nairobi, Marimba Publications.

Mohamed S.A (2001) *Jicho la Ndani*. Nairobi, Longhorn Kenya.

Monaghan, J. (1987) *Grammar in the Construction of Texts*. London, Frances Pinter.

Msokile, M (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi East Africa Educational Publishers.

Mulila, A (2005) Muala na Mshikamano katika Kiswahili: Umuhimu wake katika uchanganuzi wa riwaya ya *Vipuli vya Figo*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mutiso, K (1986) *Mizani Yangu.* Nairobi, Kenya Literature Bureau.

Neubert, T na Shreve, G (1992) *Translation as a Text*. London Kent University Press.

Njogu, K *et al.* (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Njue, J (1989) Muala katika Kiswahili: Umuhimu wake katika uchambuzi wa ngano za Kiswahili. Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Nzuki, K. (2003) Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka Mberia. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Onguko, S. (1999) A Comparative Study of Cohesion in Academic and Newspaper Texts. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Wales, K. (1989) *A Dictionary of Stylistics*. London, Longman.

Wamitila K (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

__________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi, Focus Publications Ltd.

Wangari, M (1988) New Trends in Ushairi. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Werth, P (1984) *Focus, Coherence and Emphasis*. London, Helm Ltd.

Yule, G (1985) *The study of Language.* UK, Cambridge University Press.

Yule, G. (1996) *Pragmatics.* New York, Oxford University Press.